

SAUTI YA ILE ISHARA

 Endeleeni tu kusimama kwa dakika chache tu Mbele za Bwana. Hebu na tusome kutoka kwenye Neno Lake, katika Kutoka, mlango wa 4.

...Musa akajibu akasema, Lakini, tazama, hawataniamini, wala hawataisikia sauti yangu; maana watasema, BWANA hakukutokeaa.

BWANA akamwambia, Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako?... akasema, Ni fimbo.

Akamwambia, Itupe chini; akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake.

BWANA akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, kamshike mkia; (akaunyosha mkono wake akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake;)

Ili kwamba wapate kusadiki ya kwamba BWANA, Mungu wa baba zao, Mungu wa Ibrahim, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amekutokeaa.

BWANA akamwambia tena, Sasa tia mkono wako kifuani mwako. Akautia mkono wake kifuani mwake; naye alipoutoa, kumbe! mkono wake ulikuwa una ukoma, umekuwa mweupe kama theluji.

Akasema, Tia mkono wako kifuani mwako tena. Akautia mkono wake kifuani mwake tena, na alipoutoa kifuani mwake, kumbe! umeirudia hali ya mwili wake.

Basi itakuwa, wasipokusadiki, wala kuisikiliza sauti ya ishara ya kwanza, wataisikiliza sauti ya ishara ya pili.

Kisha itakuwa wasipokuamini, hata ishara hizo mbili, wala kuisikiliza sauti yako, basi, yatwae maji mtoni uyamwage juu ya nchi kavu, na yale maji uyatwaayo mtoni yatakuwa damu juu ya... nchi kavu.

² Na tuinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi. Sasa je! una haja, jioni hii ya leo, ambayo ungetaka kumjulisha Bwana, inua tu mikono yako na useme, “Bwana, nikumbuke sasa. Nina haja.”

³ Baba yetu wa Mbinguni, tunakukaribia tena jioni ya leo, tukitambua ya kwamba tunapoinamisha vichwa vyetu kuelekea kwenye udongo tulimotoka, na, kama ukikawia, tutarudi mavumbini. Lakini tukiwa na tumaini lenye baraka la ahadi iliyo ndani ya Kristo, kwamba wote wao walio katika Mungu Kristo atawaleta pamoja Naye. Tu—tunakushukuru kwa ajili ya

ahadi hii tukufu. Na ninaomba, Mungu, kwamba utamkumbuka kila mmoja wao walioinua mikono yao, wangui pia, Bwana.

⁴ Ninaomba, usiku wa leo, ya kwamba katika kufungwa kwa majira haya ya imani, kwamba utawapa watu imani kubwa sana usiku wa leo, kwamba Bwana Yesu atakuwa halisi sana kwa kila mmoja wetu, hata hakutakuwako na mtu mnyonge mionganini mwetu baada ya usiku wa leo. Jalia kila mwénye dhambi atambue ya kwamba yeeye yuko Mbele za Bwana Yesu, na ndipo atatubu dhambi zake, na kuutoa moyo wake Kwako, na kujazwa na Roho; katika massaaya maovu ya mwisho, tunapoyaona kama kivuli kikubwa mno kinachotambaa juu ya nchi.

⁵ Tunaomba, Mungu, kwa uongozi wa Kiungu, usiku wa leo, kwa ajili ya kunena na kusikiliza. Jalia Roho Mtakatifu auchukue mkutano sasa na kuuvunja Mkate wa Uzima kwa kila mmoja wetu kadiri tulivyo na haja, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁶ Ninatumaini ya kwamba usiku wa leo tutaweza kutimiza kile tunachojaribu kuwafanya watu kuona, u—uhakika wa kumwamini Mungu.

⁷ Sasa, kesho alasiri saa nane na nusu, wote hao walio na kadi za maombi wataombewa. Halafu kuhakikisha ya kwamba hakuna mtu aliyeachwa nje, bila ya kadi za maombi, kila usiku sisi husambaza kadi za maombi. Naye atazisambaza tena kesho, mnamo...Ninadhani, mnamo saa saba na nusu ama kitu kama hicho, kabla tu ya mkutano kuanza. Na wote wanaotamani kuombewa, yejote wa wapendwa wenu, hebu na waje na wachukue kadi ya maombi. Hakika wata—watapewa kadi ya maombi. Nasi tutaninii...

⁸ Nitawaombea hao watu, kwa kuwawekea mikono na kuwaombea. Sasa kama imani yako haiwezi kuinuka katika Uwepo wa Bwana Yesu na kumpokea kama mponyaji wako, na unaamini ya kwamba kama tungeomba na kukuwekea mikono, ya kwamba hilo lingesaidia, vema, hakika tupo hapa kufanya jambo lolote unalotaka.

⁹ Sababu ya kuliahirisha mpaka kulichelewesha, muda mrefu, kuona kwamba kila mmoja ambaye ningeninii, ambaye angeweza kumfikia na kumpata Mungu kwenye misingi hiyo. Na hatuna wengi mno. Kuna ninii...Jengo hili si kubwa, na kwa hiyo hatuna watu wengi mno. Nasi tunaweza kuchukua kesho alasiri na kuwaombea wote tulio nao hapa, tikitenga alasiri hiyo kwa kusudi hilo, kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa.

¹⁰ Nasi tupo hapa kufanya lolote tuwezalo kusaidia kuyafanya maisha kidogo bora zaidi kwenu, kuwapunguzia mzigo, katika safari hii tunayosafiri.

¹¹ Na kisha wakati wowote, ambapo mtu ye yeyote anajisikia ya kwamba—ya kwamba wangetaka kumjia Bwana Yesu, haidhuru ni sehemu gani ya ibada inayoendelea, wewe njoo papo hapo. Usingojee mpaka wito wa madhabahuni utakapofanywa. Usingojee mpaka mwaliko utakapotolewa. Wewe njoo papo hapo, mkubali Kristo, na uje moja kwa moja huku na umkiri papo hapo. Kwa kuwa hilo ndilo kusudi letu kuu la kuwapo hapa, ni kuona nafsi zikizaliwa katika Ufalme wa Mungu.

¹² Na sasa, kesho ni Jumapili, na kutakuwa na shule ya Jumapili, makanisa. Sababu ya sisi kuwa na ibada zetu wakati wa alasiri, Jumapili, ni kusudi tusikatize ibada yoyote hata kidogo. Tunaamini ya kwamba kila Mkristo anapaswa kuwa na kanisa la nyu—nyumbani wanalohudhuria. Kila Mkristo anapaswa kukutana mahali fulani na waaminio. Na popote mnapokutana, hilo ndilo kanisa.

¹³ Sasa, kama ningekuwa ninaishi hapa, ningekuwa mshiriki wa moja ya makanisa haya hapa, ambayo wachungaji hawa hapa, wanaoshirikiana, wanayawakilisha. Kwa nini? Kwa sababu wako hapa wameketi jukwaani, wapate kuonekana na watu wote, ya kwamba wanakubaliana na yale yanayoendelea. Wanaiamini huduma ya namna hii, uponyaji wa Kiungu, Ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kadhalika. Wapo hapa wakiushuhudia. Wao ndio walionalika kuja hapa, kwamba huenda ikawa huduma ambayo Bwana amenipa ikalisaidia kusanyiko lao.

¹⁴ Sasa huyo ni mchungaji halisi, ambaye anatafuta baraka zote za kiroho anazoweza, za kila kitu anachofanya Mungu, kwamba anajaribu awezavyo kulisaidia kanisa lake kupiga hatua kwa Mungu. Hakika ninavua kofia yangu kwa heshima ya mchungaji kama huyo.

¹⁵ Na watu hawa iliwabidi kufanya hilo kwa shida, pia. Mnaweza kuamini hilo kuwa ni kweli. Iliwabidi wafanye hivyo kwa shida. Na mimi—mimi hakika ninashukuru kwa ajili ya watu wa Mungu walio mashuhuri hivyo, ambao wako tayari kuchukua nafasi yao na jukumu lao juu ya imani zao, na—na kuamini. Mungu na adumu kuwabariki!

¹⁶ Nami nina hakika watawafaa. Sasa, kama u mgeni hapa, tafuta kujua mahali ndugu hawa walipo na makanisa yao, mahali walipo. Watembeleeni kesho. Watakuwa na ibada maalum, na wapo wahudumu hapa watakoahubiri kwenye makanisa mbalimbali, na vile vile kama ilivyokwisha kutangazwa. Kwa hiyo iweni kule kesho.

¹⁷ Na halafu kesho alasiri, kama mngetaka kuja kwenye ibada ya mwisho, hakika tutafurahia kuwa nanyi. Makanisa yote, madhehebu yote, ni kwa ajili ya kila mtu. Kila mtu anakaribishwa; Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mpentekoste, kanisa la Kristo, kanisa la Mungu, Mkatoliki,

Myahudi Mwothodoksi, kafiri, chochote ulicho. Sisi ni... Mmekaribishwa.

“Ati unasema, ‘Kafiri?’” Naam, bwana.

¹⁸ Kama kafiri ataingia mkutanonni na kuketi chini na kujiheshimu, yeye anakaribishwa tu kama mtu mwingine yeyote. Kweli. Jambo fulani, hilo ndilo tunalomtakia hapa, kwamba jambo fulani lingetendwa ambalo lingemsaidia kuona kosa lake, na kumjia Bwana. Kwa kuwa sisi... Hakika.

¹⁹ Ni wangapi wamepata kusoma lile ono dogo ambalo gazeti la Wafanyabiashara Wakristo walichapisha, na ninaamini magazeti mengine zai-..., la, *Kuangalia Ng'ambo ya Pazio La Wakati?* Sasa hiyo ni kweli, rafiki. Usithubutu kukosa hilo. Ni—nimekuwa mtu wa tofauti tangu wakati huo. Ninajua kwamba hilo ni halisi, kwa hiyo ni—ni—ninatumaini tu ya kwamba hakuna mmoja wenu atakayekosa Mbingu hiyo kuu ambayo Mungu anayo kwa ajili ya waaminio. Kama ukiikossa, basi umefanikisha kitu gani hapa duniani? Maana, hujui ni wakati gani itakubidi kuondoka humu ulimwenguni. Lakini unajua jambo moja, hakika itakubidi kuuacha. Kwa hiyo kama hiyo ni kweli, basi si tungekuwa wajinga mno kujaribu ku—kuninii tu... Hatuthubutu kubahatisha hata kidogo. Mnaona, kumbukeni tu, aminini Neno la Mungu na kila ahadi ndani Yake.

²⁰ Wazieni tu, ni kitu gani kilichosababisha kila ugonjwa, kila huzuni ya moyoni, kila kifo, kila shida, kila huzuni, maskini mtoto huyu mdogo mwenye kifafa, mambo haya yote, walemavu, vipofu, kujengwa kwa kila hospitali? Kwa sababu mtu mmoja alikosa kuamini sehemu moja ndogo ya Neno. Huyo alikuwa ni Hawa. Shetani alilifunika tu kwake. Si kunukuu, bali alilifunika, kasema, “Hakika... Bwana ni mwema kupita kiasi.”

²¹ Unasikia sana siku hizi kuhusu ninii kuwa, Mungu kuwa Mungu mwema. Yeye ni Mungu mwema, bali kumbuka Yeye ni Mungu wa utakatifu, Mungu ambaye hawezi kupuuza dhambi. Adhabu imelipiwa, nawe inakubidi kukubali hilo juu ya misingi Yake. Pia kumbuka, Yeye ni Mungu mwenye ghadhabu, Mungu mwenye hasira. Nawe utasimama mbele ya Mungu mwenye hasira, sio tu Mungu wa wema na rehema. Usiku wa leo Yeye ni Mwokozi wako; Siku hiyo Yeye atakuwa Hakimu Wako.

²² Kwa hiyo hakikisha ya kwamba huachi hata jambo moja lisilotimizwa, rafiki. Haita—haitaninii... Hailipi kitu. Usi—usiliendee vivi hivi tu. Kuwa na hakika, hakika kabisa, kwa maana hupati nafasi nyngine. Hii ndiyo nafasi yako ya pekee, wakati ukiwa hapa duniani.

²³ Kumbuka yule tajiri na Lazaro, kulikuwako na ghuba kubwa kati yako na Yeye, ambayo hapana mtu amepata kuivuka, wala atakayepata kuivuka. Unaona? Wakati u-wakati ukifa, hakuna jambo lingine tena. Ninajua watu wanadai ya kwamba wanawenza kukuombea ukarudi kutoka sehemu hizo,

bali kamwe usiamini jambo hilo. Hilo ni kinyume cha Neno la Mungu. Unaona? "Jinsi mti unavyoegemea, hivyo ndivyo unavyoanguka." Naye Yesu alisema, Yeye Mwenyewe, ya kwamba, "Kulikuwako na ghuba, ambayo, mtu alipokufa na kwenda kuzimu, asingeweza (kamwe) kuja Mbiringuni. Hakuna mtu aliyepata kulivuka, wala hakuna angeweza." Hilo linamaliza mambo, nijuavyo mimi. Wakati Yesu aliposema hilo lilimaliza kila kitu, hakuna lingine.

²⁴ Kwa hiyo kumbuka tu, sasa ndiyo nafasi yako, na usiku wa leo huenda ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho.

²⁵ Ungeweza kung'amua kile kinachoendelea? Laiti ungaliweza tu kuliona! Ninatumaini huwazii ya kwamba nikizungumza namna hiyo, ya kwamba ninajaribu kukushawishi kumwangalia mtu fulani, ama kumwamini mtu fulani. Sifanyi jambo hilo, ewe rafiki. Ninajaribu kukufanya uamini ni Nani huyo tuliyi mbele Zake sasa. Yesu Kristo, Mungu yeye yule atakayekuhukumu kwenye Siku ile, yupo hapa akijitambulisha Mwenyewe mbele zako, jambo lile lile aliloahidi ya kwamba angefanya katika siku hizi za mwisho.

²⁶ Ninafikiri Ndugu Price, asubuhi ya leo kwenye kiamshakinywa, alitoa mfano mzuri wa kufikia kwenye kona, ndipo inakubidi kukata kona. Je! mliufurahia huo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika mliufurahia. Uliwekwa vizuri sana, sana.

²⁷ Sasa, kwa hiyo kumbukeni, mara nytingine kwenye kona, lakini hebu na tukumbuke inatubidi kupiga kona hizi. Nililhubiri juu ya huo, wakati mmoja, na kuuita, *Njia Panda*. Tunapofika kwenye njia panda, mara nydingi, inatubidi kwenda *hivi* na kwenye njia mbalimbali.

²⁸ Sasa usiku wa leo, kwa dakika chache zifuatazo, ninataka kuchukua somo hili la—la: *Sauti Ya Ile Ishara*. Na sasa tukio letu linafunguwa, usiku wa leo, katika Kitabu cha Kutoka, na *kutoka* maana yake ni "kutoka nje; kutolewa." Sasa jaribu kusikiliza kwa makini uwezavyo.

²⁹ Ningetaka kuwashubiria wakati mmoja, ninyi ni wasikilizaji wazuri sana, bali sina tu sauti. Kidogo ina uchovu, na ninajua jinsi ingekuwa. Inanibidi kupumzika kidogo sasa, kwa yapata siku nane ama kumi, kabla sijaanza mukutano ufuataao. Unaona, si mukutano huu mmoja tu hapa. Ni mukutano, siku baada ya siku, juma baada ya juma, mwezi baada ya mwezi, mwaka baada ya mwaka, unaona, hebu wazia.

³⁰ Na wazia juu ya nyakati zote, mwaka baada ya mwaka, hapajakuwapo na wakati mmoja Yeye amesema jambo lolote ila lile lililokuwa ni kweli kabisa, kamilifu; katika lugha zote, kote ulimwenguni, mara saba. Unaona? Hakuna mtu, popote, anayeweza kusema ila kwamba limekuwa kamilifu, kwenye alama hasa, kila wakati. Anaposema jambo fulani litatukia,

lilitukia vivyo hivyo hasa. Analisema kwa majuma na miezi, hata na miaka, pia, kabla halijatukia, na daima ni kamilifu kabisa kwenye alama. Kamwe halijashindwa hata wakati mmoja, wala kamwe halitashindwa, maana huyo ni Mungu. Sasa, mimi ninaweza kushindwa, kama mwanadamu. Kamwe usiniangalie kama mfano, kwa sababu mimi—mimi ni kama wewe tu, mwenye dhambi tu aliyeokolewa kwa neema. Lakini huyo ni Mungu, wa kimbunguni, unaona, akijitambulisha Mwenyewe. Haimbidi kufanya jambo hilo, bali Yeye aliahidi atalifanya.

³¹ Yesu aliponya kwa sababu huenda likitimiza Neno. Yeye alifanya mambo hayo kwa ajili kwamba Neno la Mungu lingetimizwa.

³² Hiyo ndiyo sababu Yeye analifanya leo, Neno lipate kutimizwa, ambalo nimewanukulia, usiku baada ya usiku.

³³ Sasa angalia basi wakati Uwepo Wake ukiwa karibu, Huo, hakika unasababisha mhemuko. Kama nilivyosema asubuhi ya leo, “Chochote kisicho na mhemuko kimekufa.” Na dini yoyote isiyo na mhemuko fulani ndani yake, afadhalii uizike, imekufa. Inaleta mhemuko. Yeye hutuhuisha. Lakini tukiisha kuhuishwa, hebu na tukumbuke ni Kitu gani kilichotuhuisha. Ni kitu gani kilichofanya jambo hilo? Ni Uwepo wa Roho Mtakatifu, Yesu Kristo katikati yetu, akijionyesha Mwenyewe kwamba Yeye yu hai. Si mwili wa kawaida; wakati wakati huo, mwili huo wa kawaida utakaporudi kutoka Mbininguni, hakutakuwa na wakati baada ya hayo. Hakuna lingine. Nasi tunajua ya kwamba tuko katika, tunaishi katika siku za mwisho, ambapo mambo haya yanapaswa kutukia.

Sasa, Mungu amekuwa na kutoka hapo awali. Kuna . . .

³⁴ Kila kitu kinasafiri katika tatu, kwa Mungu. Mungu anakamilishwa katika tatu. Kuja mara ya kwanza kwa Kristo, *kumkomboa* Bibi-arusi Wake; kuja mara ya pili kwa Kristo, *kumpokea* Bibi-arusi Wake; kuja mara ya tatu kwa Kristo, *pamoja* na Bibi-arusi Wake, kutawala katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Kila kitu kinafuatana katika hatua tatu.

³⁵ Sasa, kumekuwako, kutakuwako, kutoka kutatu. Kumojja kwa huko, Mungu aliwaingiza *ndani* ya safina, kwa ajili ya kutoka, kubebwa juu ya nchi. Mara ya pili, Mungu *aliwatoa* Mi—Misri. Na wakati ujao, Mungu anawatwaa *juu*. Kuingia, kutoka, kwenda juu! Kutoka kunakofuata ni kwenda juu. Tunakabiliwa na kumoja sasa, wakati wa kutwaliwa juu.

³⁶ Vile vile kama vile uhai unavyofanya jambo lile lile. Tunakuja *katika* uhai, *tunatoka* katika uhai, tukafufuka *tukawa* hai, jambo lile lile hasa. Kwa hiyo tunaninii . . .

³⁷ Tukio letu linafunguka usiku wa leo katika kutoka, naye Mungu alikuwa akijiandaa kulichukua taifa Lake.

³⁸ Israeli ni taifa. Mungu hashughulikii Israeli kama mtu mmoja binafsi. Israeli ni taifa, daima aliwashughulikia. Na katika siku za mwisho, baada ya ku—kuondoka kwa kanisa, ndipo Mungu atawaokoa Israeli kama taifa. Wako kwenye nchi ya uenyeji wao sasa, wakiwa tayari kwa jambo hilo. Nao wataokolewa, Biblia ilisema, “Taifa litazaliwa katika siku moja.” Mungu hawashughulikii Wayahudi kama mtu mmoja binafsi. Anawashughulikia kama taifa, Israeli, daima, kwa sababu ndilo taifa Lake.

³⁹ Na hapa Yeye anajiandaa kulitoa taifa Lake kutoka katika taifa, katika kutoka, kuwatoa watu Wake katika hukumu.

⁴⁰ Na maji yale yale yaliyouzamisha ulimwengu, yalimwokoa Nuhu. Mnaona? Na Roho Mtakatifu yeye yule, ambaye watu wanamkataa leo, atalipokea Kanisa na kulipeleka juu, na kushusha hukumu juu ya wasioliamini. Yesu alisema.

⁴¹ Walipomwita, “Beelizebuli,” kwa maneno mengine, “Yeye alikuwa mpiga ramli.” Wao . . .

⁴² Yeye alisema, “Nitawasamehe kwa jambo hilo,” Mwana wa Adamu. Dhabihu haikuwa imetolewa. “Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi Yake halitasamehewa katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.” Halina budi kukataliwa, na ndipo hukumu inapiga baada ya jambo hilo. Unaona, shida ni kwamba sisi . . .

⁴³ Inanikumbusha juu ya hadithi moja niliyosoma wakati mmoja, ya baharia mzee akitoka baharini, na m—mshairi kijana Mwingereza alikuwa akienda baharini. Na kwa hiyo mshairi alikuwa ameandika mengi kuhusu bahari, bali hakuwa amewahi kuiona, kwa hiyo alikuwa akienda zake kule. Ndipo yule baharia stadi akamwambia, akiwa na kiko chake cha kishungi mdomoni mwake, akasema, “Waenda wapi, jamani?”

⁴⁴ Yeye akasema, “Ninashuka kwenda baharini.” Akasema, “Sijapata kuiona. Nimeandika habari zake, na yale wengine waliyosema, lakini,” kasema, “loo, nimesisimkwa sana kujua ninakaribia baharini.” Akasema, “Loo, kunusa maji yake ya chumvi! Kuona mawimbi yake makubwa, meupe yakipasuka kwenye kilele chake, na mbingu za bluu zikijakisi, na kuwasikia shakwe wanaporuka juu yake, loo, ninasisimshwa na wazo la kuiona!”

⁴⁵ Maskini yule baharia stadi akasema, “Nilizaliwa mle, miaka sitini iliyopita, sioni chochote kilicho kizuri sana kuihusu.” Unaona, alikuwa ameionna sana hata ikawa ni kitu cha kawaida kwake.

⁴⁶ Sasa hiyo ndiyo shida ya kanisa la Pentekoste leo. Limeona mambo mengi sana ya Mungu, hata Mungu amekuwa wa kawaida kwao. Kamwe msiache hilo litukie!

⁴⁷ Hapa si muda mrefu uliopita, huko Louisville, Kentucky. Ninakotoka, Jeffersonville, Indiana, ni upande wa pili wa mto kutoka kwake. Bibi mmoja alikuwa akitembea katika duka la senti kumi. Naye (aliwuwa) alikuwa na mvulana mdoog mkononi mwake, naye alikuwa akienda kwenye kaunta na kushikwa na mpagao. Angechukua kitu fulani, akamwonyesha mvulana huyo mdoog; yeze angeketi tu na kukodoa macho. Angeenda kwenye kaunta nyingine, na kuchukua kitu fulani kumwonyesha mvulana huyo mdoog; angekodoa macho tu. Na baada ya kitambo kidogo, alichukua kengele ndogo na kuanza kuipiga, naye mvulana huyo mdoog akakodoa macho tu. Ndipo mama akaanza kupiga mayowe, na kutupatupa mikono yake. Na watu waliokuwa kwenye duka hilo la senti kumi walikuwa wakimwangalia, kwa hiyo wakamwendea wapate kujua kulikuwa na shida gani.

⁴⁸ Akasema, "Nimeninii . . . Mvulana wangu mdoog," kasema, "yeze ana umri wa miaka mitatu tu." Kisha akasema, "Mimi . . . Ghafla tu, yapata mwaka mmoja uliopita, yeze alianza kuketi tu na kukodoa macho angani." Na akasema, "Ni—nilimpeleka kwa daktari," kisha kasema, "naye daktari akaagiza matibabu fulani na kadhalika." Kisha kasema, "Naye daktari aliniambia, leo, ya kwamba alidhani alikuwa na nafuu zaidi. Lakini," kasema, "yeze hana nafuu." Kasema, "Nimetikisa kila kitu mbele zake, ambacho kinapaswa kumvutia mvulana mdoog wa umri wake, kuvutia usikivu. Kila kitu ambacho kingeweza kumvutia mtoto mdoog wa umri wake, nimekitikisa mbele zake, naye anaketi tu na kukodoa macho angani." Kasema, "Hajapata nafuu."

⁴⁹ Hicho ni kitu kama kanisa la Kipentekoste. Mungu ametikisa kila kipawa, katika Biblia, mbele zao, nao wangali wanaketi na kukodoa macho angani, kana kwamba kulikuwa na kasoro fulani. Wakati umewadnia wa sisi kuamka, enyi marafiki, kabla haijachelewa kupita kiasi. Kumbukeni, Mungu hatikisi karama hizo isipokuwa awe anajaribu kuvutia usikivu wako.

Mungu alikuwa akitoa taifa kutoka katika taifa.

⁵⁰ Kama vile tu anavyofanya sasa, kwenda kumleta Bibi-arusi kutoka katika kanisa, akiacha mabaki ya uzao wa mwanamke. Wateule watatolewa kutoka kwenye kanisa. Kanisa la kawaida litaendelea kuwa hapa katika wakati wa ile dhiki. Hao *wateule* mara nyingine wanaitwa "waliochaguliwa, wateule, mabaki."

⁵¹ Hebu na tuangalie jinsi alivyofanya jambo hilo basi, kwa kuwa Yeye habadilishi njia Yake ya kufanya mambo. Mungu anayo njia moja ya kufanya mambo, na hiyo ndivyo anavyofanya, na hiyo ndiyo njia ya kweli, daima. Tuangalie vile alivyofanya, na jinsi alivyofanya, ndipo tunaweza kupata fununu ya jambo hili.

⁵² Sasa, mimi ni muainishaji, hakika. Sina elimu. Inanibidi kuangalia nyuma na kuona jinsi Yeye alivyofanya. Nasi

tunafundishwa ya kwamba, "Agano la Kale lilikuwa ni kivuli cha mambo yatakayokuja." Kwa hiyo kama niliangalia hapa na sikuwa nimeuona mkono wangu, nami nikaona kivuli cha mkono wangu, na nilikuwa na vidole vitano, ningekuwa na fununu nzuri ya kwamba mkono wangu ulipofika pale, nilikuwa na vidole vitano. Kwa hiyo kilichowapata kilikuwa ni mifano ya jinsi Mungu anavyotenda mambo, jinsi anavyoyatenda sasa.

⁵³ Na jinsi anavyolifanya, Yeye kamwe habadiliki kutoka kwa hilo. Kila wakati, kote katika Biblia, Yeye kamwe habadilishi njia yake ya kutenda mambo. Daima ni vile vile, kwa maana njia Yake ya kwanza ya kufanya jambo hilo ndiyo njia kamilifu. Kwa sababu, Yeye asingekuwa na njia nyingine, kwa kuwa Yeye ni mkamilifu, na, Yeye, njia Zake zote ni kamilifu. Angalia jinsi alivyolifanya.

⁵⁴ Musa aliitwa na kuchaguliwa kuchukua kazi hii aliyokuwa nayo, aliyokuwa—aliyokuwa amechukua. Mungu . . .

⁵⁵ Sasa, nafikiri, kama mtaruhusu jambo hilo . . . Sisemi hili kwa kuumiza. Ninasema tu, katika jukwaa hili, si—sijui kitu wala sitaki kujua kitu ila Mungu. Sasa, nafikiri hapo ndipo ndugu zetu wa Mvua ya Vuli walipochanganyikiwa, mnaona, wanawewekeana mikono na kuwafanya manabii na kadhalika. Sasa, hilo si la Kimaandiko. "Karama na miito havina majuto." Unazaliwa chochote ulicho. Wewe uko, hapo mwanzo, kile ulicho.

⁵⁶ Waangalie hao Mafarisayo katika siku zilizopita. Walikuwa tu na nuru kidogo, kwa sababu wangeweza . . . walikuwa na torati, nao waliishi kwa torati, bali huko ndani ya moyo wao kulikuwa na giza kulivyoweza kuwa.

⁵⁷ Na kulikuwako na maskini mwanamke mmoja, kahaba, ninii yake . . . maisha yake ya hapo nyuma *hapa* yalikuwa ni meusi yawezavyo kuwa, alikuwa na sifa mbaya, bali huko ndani ya moyo wake yeye alikuwa amechaguliwa tangu zamani kwa ajili ya Uzima.

⁵⁸ Ndipo basi wakati Yesu, lile Neno, alipojitokeza jukwaani, hao Mafarisayo walisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli." Jambo hilo lilifanya nini? Lilitia giza ile nuru ndogo waliyokuwa nayo.

⁵⁹ Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi, na kazi zake mnazifanya."

⁶⁰ Bali wakati maskini mwanamke huyu mchafu alipokuja, naye akaliona Neno la Mungu, yeye alilitambua. Hakuliishi, bali alilitambua. Na mara tu liliposema naye, yeye alisema, "Naona ya kuwa U Nabii." Na Yeye . . . Huyo mwanamke akasema, "Ninajua Masihi atafanya jambo hili."

Ndipo akasema, "Mimi Ndiye."

⁶¹ Lilifanya nini? Lilisafisha weusi huo na kuufanya wote mweupe. Kwa nini? Kulikuwako na mbegu iliyoukuwa imekaa

pale, mbegu iliyochaguliwa tangu zamani iliyokuwa katika... Lilikuwa ni wazo la Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

⁶² Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Kama una Uzima wa Milele, basi wewe mwenyewe ulikuwa katika mawazo ya Mungu kabla ulimwengu haujaumbwa. Wewe ni sifa za mawazo Yake, maana Milele kamwe haikuanza wala kamwe haiwezi kuisha. Wewe ni sehemu ya uchumi wa Mungu, daima. Inaakisi tu. Inageuka sasa. Wana picha moja zaidi ya kusafisha, hiyo ni mauti, ndipo negetivu itakuwa kitu chenyewe, ndipo uko katika Bibi-arusi na pamoja na Kristo, kama Yeye alivyowazia. Kama vile mume na mke, leo, ndivyo (Mungu) Kristo na Kanisa watakuwa kitu kimoja. Sasa, wateule, walioitwa!

Musa alizaliwa, "mtoto anayefaa." Biblia ilisema hivyo.

⁶³ Mmoja wa manabii, Yeremia. Mungu alisema, "Kabla hata hujauambika katika tumbo la mama yako, nilikuchagua kuwa nabii kwa taifa."

⁶⁴ Yohana Mbatizaji, mbona, ye ye alitambulishwa katika Maandiko. Isaya, miaka mia saba na kumi na miwili kabla ya kuja kwake, alisema, "Yeye ni sauti ya mtu aliaye nyikani, 'Itengenezeni njia ya Bwana!'" Na yapata miaka mia nne kabla ya kuonekana Kwake, tena tunaona, Malaki alisema, "Tazama ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia mbele za Bwana."

⁶⁵ Unaona, ye ye alichaguliwa tangu zamani. Na vivyo hivyo ofisi hizo zote za Mungu, endapo wameitwa na Mungu.

⁶⁶ Kama wameelimishwa ili kufanya jambo hilo, ni chakula tu cha mzinga, unaona, hawawezi kuwa kitu chochote. Kama ni tikiti ya posho, basi mnaiza haki zenu za kuzaliwa kwa tikiti za posho, utapatana upate kwenda pamoja na madhehebu ama kundi fulani. Bali kama ni suala la Mungu, utasimama pamoja na hilo Neno, haidhuru, kwa sababu ulizaliwa upate kusimama nalo.

⁶⁷ Musa, hakuna mtu mwingine angeliweza kupachukua mahali pake. Hakuna mtu mwingine angeliweza kufanya kazi hiyo. Alichaguliwa kuifanya.

⁶⁸ Na, ndugu, dada, kama una Uzima wa Milele, ulichaguliwa kufanya jambo fulani. Labda mke mzuri wa nyumbani, labda kitu kingine, bali hakuna mtu anayeweza kupachukua mahali pako. Mungu amekufanya mahali. Usijaribu kupachukua mahali pa mtu mwingine. Huo ni uigizaji wa kimwili, unaona, inaonyesha una kasoro fulani. Kuwa jinsi ulivyo, vivyo hivyo hasa. Usiwe kitu kingine tofauti.

⁶⁹ Sasa, sasa tunaona ya kwamba Mungu alimpa Musa ishara apate kuthibitisha madai na miito.

⁷⁰ Na kila ishara ya kweli, kila ishara ya kweli, inayotumwa kutoka kwa Mungu, ninii . . . ina sauti nyuma yake. Sasa usikose. Hili ndilo somo langu la mwisho juu ya jambo hili, unaona. Kila ishara ya kweli . . . Sasa tuna ishara zisizotoka kwa Mungu; Shetani anaweza kuiga karibu chochote kilichoko. Lakini ishara ya kweli, iliyotumwa kutoka kwa Mungu, ina sauti ya Mungu nyuma yake.

⁷¹ Mungu alimwambia Musa, “Wasipoiamini sauti ya ishara ya kwanza, basi fanya ishara hii nyingine mbele zao. Ndipossa wasipoisikia hiyo, chukua tu maji na uyamwage juu ya nchi.” Na hiyo ilikuwa ni ishara ya kwamba wataloweshwa mle katika damu yao wenyewe.

⁷² Angalia, na ni vile tu Yeye alivyo sema, “Kung’uteni mavumbi ya miguuni mwenu. Ingekuwa rahisi kwa Sodoma na Gomora kustahimili, siku hiyo, kuliko itakavyokuwa kwa mji huo utakaowakataa.”

⁷³ Sasa hatuliigizi Kanisa. Hili *ni* Kanisa. Kristo ndiye Kanisa. Tumo ndani ya Kristo. Mwili wa kisiri wa Kristo, tunazaliwa ndani Yake. Huwezi kujiunga Nalo.

⁷⁴ Nimekuwa na familia ya Branham kwa karibu miaka hamsini na mitano, wala kamwe hawakuniomba kujiunga na familia hiyo. Nilizaliwa Mbranham.

⁷⁵ Na hivyo ndivyo ulivyo Mkristo. Unazaliwa Mkristo, sio kuunganishwa humo nalo. Unazaliwa ndani yake. Kila mtu anaogopa kule kuzaliwa. Wana njia safi ya kuchukua maskini mkono mdogo, ama kuweka sahihi kwenye kadi ndogo, ama kidau cha chumvi chenye maji ndani yake. Huko siko kule kuzaliwa. Kuzaliwa ni jambo la kutisha. Kuzaliwa ni ja—jambo la kuogofya sana. Sijali kama ni katika kizizi cha nguruwe, ama ki—ama kibanda, ama chumba kilichopambwa kwa rangi ya waridi hospitalini; kuzaliwa ni mchafuko, na kunakuchafua. Hutaki kujisalimisha, hutaki *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*, bali machozi yatasafisha rangi kutoka usoni mwako na kukufanya mtu wa tofauti. Kama ukizaliwa mara ya pili, kutakuchafua, bali utatoka ukiwa kiumbe kipyta. Unaona? Hawataki jambo hilo. Wanataka njia fulani rahisi, mwajua, wala hakuna njia rahisi. Kama vile wimbo, yeye alisema, “Nitashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa.” Hataki kuwa mmea wa kuoteshwa.

Kila ishara ya kweli ya Mungu hufuatwa na sauti ya Mungu.

⁷⁶ Sasa kama mtu akitoa ishara katika nchi, ama wakati wowote, na sauti hiyo anayosema nyuma yake si Neno la Mungu, basi tahadhari nayo, usiiamini. Kama shule fulani ya kale, kama mtu akiamka na kusema, akionyesha ishara kutoka kwa Mungu, halafu mafundisho ya mtu huyo ni theolojia ile ile ya kale ambayo mmekuwa nayo miaka hii yote, Mungu kamwe hakuituma ishara hiyo. Rejeeni kwenye Maandiko mwone kama ndivyo ilivyokuwa. Yachunguzeni Maandiko.

Jamaa huyo akirudi, na kusema, "Sasa tunataka sote tujiunge na *hili*. Limekuwa ni jambo lililowekwa msingi zamani." Kamwe msiamini jambo hilo. Tutaingilia jambo hilo, katika dakika chache tu, mnaona. La, msiamini jambo hilo.

⁷⁷ Mungu daima huthibitisha ishara Zake. Ishara inayotoka kwa Mungu daima hunena sauti ya Mungu.

⁷⁸ Na kama ni itikadi ile ile ya kale ambayo mmekuwa nayo, kwa nini Yeye atoe ishara, tayari mko ndani yake? Yeye anajaribu kuwaweka kwenye kona hiyo. Ishara ya kusimama! Kupunguza mwendo! Angalia unakoelekea! Utajitupa pembeni usipokuwa mwangalifu. Kuna kona kali, na daima kuna ishara pale kabla hujafikia kwenye kona hii, usije ukapata ajali. Mjenzi mzuri wa barabara hutoa ishara. Nasi tunasafiri kwenye barabara ya kwenda Utukufuni. Na kama ishara hiyo ikisema jambo lile lile la kale, haikutoka kwa Mungu.

⁷⁹ Mungu hutoa ishara kuvutia usikivu wa watu Wake. Ishara ni za kuvutia usikivu wa watu wa Mungu, ndivyo zilivyo ishara za Mungu. Ishara za Mungu hutolewa zipate kuuvutia usikivu wa watu wa Mungu.

⁸⁰ Sasa hapa kile kijiti kilichowaka moto kilikuwa ni ishara ya kumvutia yule nabii, ikijaribu, kwa sababu nabii huyo alikuwa amemkimbia Mungu, ndiposa Mungu akatoa ishara ya kijiti kilichowaka moto kama ishara. Naye akaona ishara hii ya ajabu; akasema, "Nitageuka nione ishara hii ya ajabu ni nini, ambapo ki—kijiti kinawaka moto wala hakiungui." Sasa Mungu alikuwa akivutia usikivu wa nabii wake mtoro. Angeweza kumchukua mwingine, bali alimchagua Musa kwa ajili ya kazi hiyo wala hakuna mtu mwingine atakayechukua mahali pake.

⁸¹ Safarini, jamaa wengine walijaribu kufanya jambo hilo, mwajua. Dathan aliinuka na alitaka kuunda dhehebu kutoka katika hilo. Mungu akamwambia Musa, "Jitenge. Nitawameza tu." Mnaona?

⁸² Mungu hufanya kazi na mtu mmoja. Unaona? Sasa angalia hii, alikuwa akijaribu kuvutia usikivu wa nabii, kumweka nabii mahali pake panapofaa, unaona, na Yeye alitoa ishara ya kijiti kilichowaka moto.

⁸³ Na, angalieni, sauti iliyoiifuata ishara hiyo ilikuwa ni sauti ya Kimaandiko. "Nimesikia kilio cha watu Wangu, na maombolezo yao, kwa sababu ya wasimamizi wao, nami ninakumbuka ahadi Yangu." Amina. Hilo latosha. "Ninakumbuka ahadi." Hiyo ilikuwa ni sauti ya Kimaandiko. "Nami ninakutuma huko. Nimeshuka kuja kuwakomboa, Nami ninakutuma."

⁸⁴ Kumbukeni, Mungu hatendi lolote nje ya mwanadamu. Mnajua jambo hilo? Hilo ndilo huwakwaza watu. Mnaona?

⁸⁵ Hilo ndilo liliowakwaza kumhusu Yesu. Walisema, "Wewe ni Mwanadamu, ukijifanya Mungu." Yeye alikuwa ni Mungu, bali

wasingeweza kufahamu jambo hilo. “Vema, Wewe, ukiwa tu ni Mwanadamu.”

⁸⁶ Yeye akasema, “Vema, mnawaita manabii, ‘miungu,’ na torati yenu ilitambua jambo hilo. Na endapo mnawaita ‘miungu,’ hao ambao walijiliwa na Neno la Mungu, mnawezaje kunihukumu Mimi ninaposema mimi ni Mwana wa Mungu?”

⁸⁷ Unaona, ishara, kuvutia usikivu. Na, kumbukeni, kama usikivu ukivutiwa, ukiwa ni mwelekeo ule ule, sio Mungu.

⁸⁸ Bali Mungu anajaribu kumvutia nabii sasa, Naye anampa ishara, na sauti iliyofuata ishara hiyo ilikuwa ni sauti ya Kimaandiko. “Nimewaona watu. Nimesikia kilio chao. Ninakumbuka ahadi Yangu.”

⁸⁹ Sasa Mungu atanena kwa Neno Lake lililoahidiwa. Hana budi kumtuma nabii Wake, kwa kuwa Neno humjia nabii. Biblia ilisema, Mungu alisema, Yeye Mwenyewe, ya kwamba, “Hatendi neno mpaka alifunue kwa watumishi Wake manabii kwanza.” Unaona? Ndiposa ishara inatolewa. Na Maandiko yanatambulishwa, hiyo ndiyo Sauti ya ishara.

⁹⁰ Je! unaona Sauti ya ishara, ya Musa? Kwanza, ishara ilikuwa ni kijiti kilichowaka moto; Sauti hiyo ilikuwa ni Maandiko.

⁹¹ Musa aliichukua hiyo kama ishara Yake, kisha akashuka kwenda Misri na kufanya ishara aliyoambiwa na Mungu; nayo ishara hiyo ilikuwa na sauti kwake, nao watu wakaamini na hao wakatoka. Na mradi walikuwa wakitembea, walifanya vema; bali walipoanza kunung’unika dhidi ya ile sauti, basi walismama.

⁹² Kumbukeni, Israeli ilisafiri. Je! mliju umbali zaidi waliosafiri? Wangeweza kuwa... Walikuwa maili arobaini tu, na karibu miaka arobaini wakifanya hivyo. Kwa nini? Ni kwa sababu walianza kunung’unika dhidi ya sauti iliyokuwa imetoa ile ishara. Hawakujua kabisa, walipokuwa wakipiga makelele kule ufukoni, na kuchenza katika Roho, na Musa akiimba katika Roho, walikuwa umbali wa siku chache tu. Bali walianza kunung’unika, na walitaka kufanya jambo fulani la tofauti; nao wakakaa miaka arobaini nyikani, na kuangamia mle, hiyo ni kweli, kwa sababu hawakuamini. Mungu alisema, “Hawazungumzi dhidi yako, Musa. Wanazungumza dhidi Yangu.” Hiyo ilikuwa ni sauti ya Mungu, si ya Musa.

⁹³ Sasa angalia, Yehova atazungumza kwa Neno Lake lililoahidiwa, kwa hiyo hana budi kuwatuma manabii Wake. Hilo, kama ukitaka kuliona hilo, hilo liko katika Mwanzo 15:16. Tunaona ya kwamba Mungu alimwambia Ibrahimu, “Uzao wako utakuwa mgeni katika nchi hii ya kigeni, nami nitawatoa kwa mkono wenye nguvu. Uovu wa Waamori haujatimia bado.” Ahadi Zake zote alizotoa, hapa Yeye anamvutia nabii, kwa kijiti kilichowaka moto.

⁹⁴ Sasa kama kijiti hicho kilichowaka moto kingalisema, “Musa, Mungu ni Mungu.”

“Naam, ninaamini hilo.”

⁹⁵ “Loo, unafanya vizuri, Musa, endelea tu. Umeoa mwanamke mzuri; ye ye ni mtoto mrembo. Hakika una mwana mzuri wa kiume! Utukufu kwa Mungu!” Hiyo ni itikadi ile ile ya kale. Mnaona?

⁹⁶ Lakini alikuwa tayari kufanya jambo fulani, kwa hiyo ilimbidi kuvutia usikivu wa mtu huyo. Naye akampa mtu huyo ishara mbili za kufanya, kisha akasema, “Kila ishara ilikuwa na sauti.” Hiyo inathibitisha kwamba ni kweli. Sasa angalia yale hizo sauti zilinena, hata uumbaji. Yehova alikuwa tayari kunena sasa.

⁹⁷ Tena, kuja kwa nabii ni ishara. Je! mlijuwa hilo? Kuja kwa nabii, kwenye wakati, ni ishara.

⁹⁸ Sasa, simaanishi Daktari wa Ungu. Simaanishi mchungaji fulani mwaminifu, mtu fulani mzuri. Hao ni sawa. Hao ni watumishi wa Mungu.

⁹⁹ Lakini nabii ni ishara. Biblia inasema hivyo hapa. Na ni ishara ya kitu gani? Ni ishara ya kwamba Neno Lake liko karibu kutimia, kutimizwa na sauti ya ishara ya nabii huyu.

¹⁰⁰ Angalia, kuja kwa nabii ni ilani ya ishara ya hukumu inayokaribia. Je! mlijuwa hilo? Hukumu iko tayari kupiga kama kuna nabii nchini.

¹⁰¹ Kumbukeni, ye ye hakika, kwanza, hana budi kuthibitishwa na Mungu pamoja na Neno la siku hiyo, ndiposa anafanya ishara. Na halafu angalia ishara hiyo, yale anayobashiri. Yeye alisema, “Kama likitimia, basi msikieni.” Hesabu 12:6. “Lisipotimia, sahau.” Ishara anayofanya inapaswa kuwa ni ya Kimaandiko.

¹⁰² Na kile anachotoa kama ishara, wakati mmoja, kama ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye anatoa ishara ile ile daima. “Neno la Bwana liliwajia manabii.” Walikuwa ni Neno. Na wakati Yesu alipokuja, Yeye alikuwa ni Neno. Nalo Neno liliyatambua mawazo na makusudi ya moyo, daima, na kuendelea. Sasa angalia.

¹⁰³ Kuja kwa nabii huyu, kunatoa ishara, ya, “hukumu imekaribia,” daima.

¹⁰⁴ Hebu na tusimame tu kwa dakika chache tu. Sitachukua muda mrefu sana. Hebu na tuwachunguze wachache sasa, kwa dakika kumi hivi. Na sehemu ya ujumbe iliyobaki, hasa, kwa dakika kumi.

¹⁰⁵ Nuhu, nabii nchini—nchini, ishara ya hukumu ijayo. Musa, nabii nchini, ishara ya hukumu ijayo. Eliya, nabii nchini, ishara ya hukumu ijayo. Yohana, nabii nchini, ishara ya hukumu ijayo kwa Israeli; walikatiliwa mbali kabisa.

¹⁰⁶ Angalia, ishara! Ishara hufanya kitu gani? Ishara ni kwa ajili ya kuvutia usikivu, na kuwatayarisha wateule, na waondoke njiani kabla hukumu haijapiga. Hivyo ndivyo Nuhu aliyyofanya, aliwatayarisha wateule. Hao wengine, na inafanya kitu gani? Hiyo ishara, na sauti ya ishara, humhukumu asiyeamini na kumwandaan kwa ajili ya hukumu. Inawafanya wateule tayari kwa ajili ya kupona. Hivyo ndivyo ishara ilivyo. Hiyo ndiyo sababu ya kutolewa kwa ishara, kwa ajili ya hukumu ijayo. Kwa wateule, wanaiona.

¹⁰⁷ Ni kama maskini yule mwanamke mwenye moyo safi, na mwili mchafu; na Farisayo mwenye mwili safi, na moyo mchafu. Ilimhukumu mmoja, na humwokoa mwingine.

¹⁰⁸ Na hukumu zile zile zilizomwokoa Musa, ziliuhukumu ulimwengu; mahubiri yake.

¹⁰⁹ Inawafanya wateule kuwa tayari. Wateule wako tayari kwa ajili ya jambo gani? Wanapoona ishara iliyotumwa na Mungu, wanarejea kwenye Maandiko na kuona kama hiyo inapaswa kuwapo. “Naam, hii hapa.” Ni kitu gani? Kusubiri hukumu. Ndipo wateule wanaisikiliza sauti hiyo.

¹¹⁰ Bali wasiotueuliwa wanaipuuu, na kusema, “Upuuzi. Endeleeni! Tutachukua shule ile ile ya kale.” Unaona? Hivyo ndivyo walivyofanya katika siku za Luther. Hivyo ndivyo walivyofanya katika siku za Wesley. Hivyo ndivyo wa-wanavyofanya sasa, vile wamefanya daima.

¹¹¹ Lakini ni ishara, na ina sauti inayoiifuata ishara. Nayu hiyo sauti inatambulikana kama sauti ya Kimaandiko. Sasa msisahau jambo hilo. Sasa endeleeni kulikoleza hilo, kwa sababu huenda nisiwaone tena.

¹¹² Laiti ningalikuwa na njia ambapo ningekuja hapa mahali fulani na kuwakusanya ndugu zangu wote, wakati hawakuwa na uamsho wowote unaoendelea, tupige hema na kuketi tu, siku baada ya siku, na kufundisha jambo hilo mpaka—mpaka limekolea hasa. Bali Yeye asingeruhusu jambo hilo, sidhani. Mnaona, tumekaribia mno mwisho. Ninaamini sasa hivi tuko mwisho kabisa.

¹¹³ Katika kitabu changu mle ndani, ambacho nimekiweka kimeandikwa. Katika mwaka wa 1933, asubuhi moja, nikijiandaa kwenda kwenye shule ya Jumapili, shule ya Jumapili ya Kibaptisti ambako nilikuwa mchungaji, Roho Mtakatifu alikuja na kunionyesha mpaka kwenye wakati wa mwisho, na akanionyesha mambo saba ambayo yangetukia. Niliyaandika. Yako kwenye karatasi ya kale ya manjano.

¹¹⁴ Aliniambia jinsi hasa Ujerumanu ingejenga ile Ngome ya Siegfried, na jinsi ambavyo Wamarekani wangepigwa vita vikali hapo, miaka kumi na moja kabla hi—hiyo ngome haijapata kujengwa.

¹¹⁵ Kasema jinsi Mussolini angeinuka, na jinsi ambavyo angeenda Ethiopia, na jinsi ambavyo Ethiopia “ingeanguka kwa urahisi mno.” Naye angekuwa kifo cha aibu, amegeuzwa kichwa chini miguu juu, na watu wake mwenyewe wangemtemea mate.

¹¹⁶ Nami nikasema, “Kuna itikadi tatu; Ukomunisti, Ufashisti, na Unazi. Zote zitaishia katika Urusi, katika Ukomunisti.” Nao utauangamiza Ukatoliki. Angalieni kama hautauangamiza!

¹¹⁷ Nilisema, “Maendeleo makubwa sana yatafanyika!” Nikasema, “Ninaona motokaa zikionekana kama yai, zikishuka kwenda barabarani. Kuna magari yanayoshuka kwenda kwenye barabara kuu, yakiendeshwa kwa njia fulani ya kidhibiti, haiwabidi kuliongoza. Niliona familia ya Kimarekani ikicheza dama nyuma ya gari.” Wanalo gari hilo sasa hivi, laiti wangalikuwa na barabara kuu za kuliweka humo. Gari dogo la Volkswagen ni yai kamili, kweli kabisa, na ndivyo yalivyo magari mengine yote. Ungeweza kuwazia, katika mwaka wa 1933, jinsi magari yalivyo kuwa, ukilinganisha na ya siku hizi?

¹¹⁸ Kisha ikabashiri tena, ya kwamba, kuwaruhusu wanawake kupiga kura, na jinsi wangefanya. Na jinsi ambavyo nchi hii, ikiwa ni mfano, kama vile Israeli, walivyoingia nchini na kuwafukuza wenyeji wake, na kuimiliki hiyo nchi. Nao wafalme wachache wa kwanza waliokuwa nao, Daudi na Sulemani, walikuwa wafalme wacha Mungu. Baada ya kitambo kidogo, walikuwa na Ahabu jukwaani. Walimpigia kura akaingia. Kiti kilininii... kanisa likawa la kilimwengu. Na, sisi tumekuwa na Lincoln na Washington, angalia jinsi mambo yalivyo leo hii. Angalieni mahali tunakoelekea sasa. Jambo linalofuata ni lipi? Tuko katika wakati wa mwisho.

¹¹⁹ Na ni ishara, katika mambo ya kawaida, hakika kabissa. Inawafanya wateule kuwa tayari; na kuhukumu, hukumuni, asiyeamini.

¹²⁰ “Kama nabii huyu ni nabii wa kweli, na asemayo yanatimia,” Biblia ilisema, katika Hesabu 12:6, “sikilizeni onyo lake, kwa kuwa imethibitishwa si mtu huyo.” Na—nabii ni mwanadamu. Lakini sauti inayotoka kwenye ishara ya kimbunguni ni sauti ya Kimaandiko, ikithibitishwa, basi ni onyo.

¹²¹ Biblia iliandikwa na manabii, kumbukeni. Katika Petro wa Pili, pia, 1:21. Katika Waembrania 1:1, pia.

¹²² Nguzo ya Moto, kwa Musa, ilikuwa ni ishara, sauti ilikuwa inaenda kunena. Nguzo ya Moto ilionyesha ya kwamba sauti ilikuwa inaenda kunena. Hiyo ni ishara, Nguzo ya Moto. Ninyi watu mnapaswa kukumbuka jambo hilo kutoka Houston, si muda mrefu uliopita.

¹²³ Musa, nabii, ishara kwa Israeli, ya kwamba ile ahadi ilikuwa tu karibu kutimizwa. Wakati Musa aliposhuka na kufanya ishara ya nabii, walijua papo hapo yeche angewakusanya pamoja.

¹²⁴ Jinsi Neno la Mungu lilivyo kamilifu katika utaratibu, kila wakati ni lile lile. Kama tu nilivyosema jana usiku, jinsi ambavyo Urimu Thumimu, na kila kitu, daima imewajibika kwa Mungu.

¹²⁵ Hebu na tumchukue nabii tena, kwa muda kidogo tu, Yona. Nilikuwa nimeandika mlango wa kwanza wa Yona hapa, mlango wa 1 hapa wa unabii wake. Yona alitoka kwenye tumbo la nyangumi, ilikuwa ni ishara. Unaona, hao watu walikuwa ni makafiri. Waliiabudu miungu ya baharini, na mungu wao wa baharini alikuwa ni nyangumi.

¹²⁶ Sasa watu wengi hujaribu kumlaumu Yona. Mimi daima nilimtetea Yona. Yona hakuwa nje ya mapenzi ya Bwana. “Hatua za mwenye haki zinaongozwa na Bwana.” Tunataka kusema, “Yeye ni Yona.” Lakini hebu na tulichukue tu katika ninii yake... thamani yake, kwanza. Ninajua alipaswa kwenda Ninawi, bali Mungu alimfanya achukue hiyo meli kwenda Tarshishi. Naye akafanya shida itokee baharini.

¹²⁷ Yona akasema, “Nifungeni mikono na miguu. Mimi ndimi mwenye shida, ndiye niliyeisababisha.” Ndipo wakamtupa nje. Na samaki alikuwa akiogelea majini, samaki mkubwa aliyemmeza Yona. Ninajua hilo ni vigumu kwa sayansi kuamini.

¹²⁸ Hapa si muda mrefu uliopita, kule Louisville, Kentucky, yapata miaka kumi iliyopita, walikuwa na nya—nyangumi juu ya m—mkokoteni. Na kulikuwako na maskini Ricky fulani kule, alikuwa na akili nyingi kuliko alivyojua jinsi ya kuzidhibiti. Alikuwa akijaribu kuifanya Biblia iseme uongo. Akasema, “Mnajua, mnaisikia ile methali ya kale ya Biblia, ya kwamba nyangumi alimmeza Yona.” Akasema, “Angalieni, msingeweza kuitisha mpira kooni mwake, ilikuwa ni dogo sana. Mtu mzima angeweza kuingia tumboni mwake?” Kasema, “Mnaona, ni methali ya kale tu, kama vile Biblia ilivyojaa hizo.”

¹²⁹ Hilo lilizidi sana mawazo ya—yangu. Nikasema, “Bwana, ningetaka kusema jambo fulani hapo.”

Kasema, “Wataka kusema nini?”

¹³⁰ Nikasema, “Unaona, hujaisoma Biblia vizuri.” Nikasema, “Biblia ilisema huyu alikuwa ni nyangumi maalum. ‘Mungu alimwandaa samaki mkubwa.’ Huyo aliundwa kwa njia maalum, apate kummeza, ambaye aliachiliwa afanye hivyo! Hakuwa ni samaki wa kawaida. Mungu alikuwa akienda kufanya kazi isiyo ya kawaida, kwa hiyo akamchukua samaki asiye wa kawaida.” Mnaona? Hakusema zaidi juu ya jambo hilo basi. Kwa hiyo, hilo, Mungu alikuwa na jambo maalum.

¹³¹ Kama vile msichana mmoja mdogo, wakati mmoja, akija kutoka maskanini; nywele zake ndogo zimechanwa kwa nyuma, na ni laini, vya kutosha mpaka maskini uso wake ulioneekana kama kitunguu kilichomenywa. Alikuwa tu na Biblia, akishuka kwenda zake.

¹³² Huyu mzee aliyeitwa Jim Dorsey aliishi huko Utica. Alikuwa kafiri, askari mzee, na—na hakumwamini Mungu. Ndipo akasema, “Waenda wapi, ewe msichana?”

Akasema, “Ninaenda nyumbani, bwana.”

Kasema, “Ni kitu gani hicho unachobeba mkononi mwako?”

Akasema, “Ni Biblia.”

Kasema, “Huiamini hiyo, sivyo?” Na huyo mzee . . .

Kasema, “Ndiyo, ninaiamini, bwana.”

¹³³ Kisha kasema, “Je! unaamini hiyo hadithi humo ndani kuhusu nyangumi kummeza Yona?”

Kasema, “Mbona, hakika, ninaamini kila Neno lake.”

¹³⁴ Akasema, “Utaithibitishaje kwa njia nytingine yoyote mbali na imani, kile mnachoita imani?”

“Mbona,” binti kasema, “nitakapofika Mbinguni, nitamwuliza Yona.” Mnaona?

Akasema, “Basi vipi kama ye ye hayuko huko?”

¹³⁵ Binti akasema, “Basi itakubidi wewe kumwuliza.” Kwa hiyo nilifikiri hicho kilikuwa ni kinyoshaji kizuri sana. Kwa hiyo nafikiri ya kwamba hiyo karibu ni kweli.

¹³⁶ Kama Biblia ilisema ya kwamba Yona alimmeza nyangumi, ningeaminjambo hilo. Ye ye angeweza kumwandaa. Yale Mungu amesema, Mungu anaweza kutimiza, Naye daima hudumisha Neno Lake. Kwa hiyo, Yona, tunamdhihaki . . .

¹³⁷ Lakini uliwahi kumwangalia samaki wakati anapoogelea? Anatafuta chakula chake. Na wakati anapokula, anashuka anaenda chini na kupumzisha mapezi yake huko chini kabisa. Mlishe samaki-dhababu wako ndipo uone lililotukia. Wanajaza matumbo yao madogo, kisha wanashuka chini na kuweka mapezi yao moja kwa moja huko chini, na kulala kule na kustarehe.

¹³⁸ Vema, samaki huyu mkubwa aliywewkwa tayari alikuja na kummeza nabii huyu. Kisha akashuka akaenda chini kabisa ya bahari, na labda mikono arobaini kwenda chini kule. Alishuka chini kabisa, akajistareheshe chini ya bahari.

¹³⁹ Sasa sisi daima tunawazia kuhusu Yona. Na kila mtu anasema, “Sasa niliombewa, bali mkono wangu haujapona. Niliombewa, bali sisikii nafuu.” Kamwe usimkemee Yona.

¹⁴⁰ Sasa angalia dalili alizokuwa nazo. Sasa, kwanza, alikuwa huko nje kwenye bahari iliyochafuka, na alikuwa ameiacha njia ambayo Mungu alikuwa amemtuma. Mikono yake na miguu yake ilifungwa. Alitupwa kwenye bahari yenye tufani, iliyochafuka, ndipo nyangumi akammeza na kushuka moja kwa moja chini ya bahari. Naye alikuwa amelala mle kwenye matapiko, katika tumbo la nyangumi, mwani umezinga shingo

yake. Na kama aliangalia upande *huu*, lilikuwa ni tumbo la nyangumi. Akaangalia *huko*, lilikuwa ni tumbo la nyangumi. Kila alikoangalia, lilikuwa ni tumbo la nyangumi. Nena kuhusu kisa cha dalili, huenda alikuwa nacho. Lakini mnajua alilosema? Alisema, “Ni ubatili wa uongo. Sitauangalia tena, bali mara nyingine tena nitatazama kuelekea hekalu Lako takatifu.”

¹⁴¹ Kwa kuwa, Sulemani, mtu wa kawaida duniani, ambaye aliomba katika kuliweka wakfu hekalu, alisema, “Bwana, kama watu Wako wakiwa katika shida mahali popote, na waangalie mahali hapa patakatifu, basi sikia kutoka Mbinguni.”

¹⁴² Naye Yona alikuwa na imani katika yale Sulemani aliyokuwa ameomba. Ndipo Mungu akamwokoa na yule nyangumi, baada ya siku tatu mchana na usiku. Huenda aliweka hema ya oksijeni kule chini. Sijui Yeye alifanya nini, bali alimhifadhi akiwa hai kwa siku tatu usiku na mchana, kulingana na Neno. Na Neno ni kweli.

¹⁴³ Vema, kama Yona, chini ya hali hizo za mambo, angeweza kuangalia tena kuelekea maskani ambayo mwanadamu alitengeneza, ni zaidi sana vipi wewe na mimi, usiku wa leo, tunavyopaswa kuangalia kwenye lile Hekalu ambamo Yesu anasimama kwenye mkono wa kuume wa Ukuu, akiwa na Damu Yake Mwenyewe, akifanya upatanisho kwa maungamo yetu, juu ya maskini dalili zetu ndogo! Usimlaumu Yona, na kisha uangalie shida yako ni nini. Iangalie ile ahadi, “Mungu alisema hivyo!” Kama ninyi ni watoto wa Ibrahimu, “Mungu alisema hivyo!” Yeye alitoa hiyo ahadi, na hilo latosha.

¹⁴⁴ Angalia, watu wote walikuwa huko nje wakivua samaki, na wakiwa wanavuta nyavu zao na kadhalika. Baada ya kitambo kidogo, huyu hapa mungu wa baharini anakuja, nyangumi, akikimbilia ufukoni. Kila mtu alipiga magoti yake. Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo. Naye akafika moja kwa moja ufukoni na kuutoa ulimi wake, na, alipoutoa, huyu hapa nabii anakuja akitembea moja kwa moja kutoka katika kinywa cha nyangumi huyo. Yule nabii! Yule mungu alimtapika nabii papo hapo ufukoni. Si ajabu walitubu. Mnaona?

¹⁴⁵ Hiyo ilikuwa ni ishara. Yona akiwasilishwa na nyangumi, alikuwa ni ishara. Yeye alifanya nini? Hiyo ilikuwa ni ishara kutoka kwa Mungu. Sauti ilisema nini? “Tubuni la sivyo mtaangamia, katika siku arobaini.” Ishara ya Mungu; sauti ya Mungu! Daima, Mungu anapotuma ishara, Mungu hutuma sauti Yake nyuma ya hiyo ishara. Angalia, “Tubuni, la sivyo katika siku arobaini jiji hili lote litaangamia.”

¹⁴⁶ Kutokea kwa nabii Yohana duniani, baada ya miaka mia nne bila nabii; ile ishara baada ya miaka mia nne, ya yeye kutokea. Maskini wakati huo mlegevu!

¹⁴⁷ Sasa kama wewe ni wa kiroho utashika ninalosema. Mungu na afungue ufahamu wako. Jinsi umekuwa ni muda mrefu!

¹⁴⁸ Miaka mia nne, Israeli bila nabii, makanisa yalikuwa yamechanganyikiwa sana, na ndipo huyu hapa Yohana anajitokeza jukwaani. Yohana alikuwa ni nabii, ishara ya kwamba Masihi yuaenda kunena baada yake. Angalia. Kwa sababu, Malaki 3 ilisema, “Nitamtuma Mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia, kuwatayarisha watu.”

¹⁴⁹ Mwangalie Yohana, hamna uchoyo ndani yake. Yeye kamwe hakuchukua utukufu wowote. Walijaribu kumwita Masihi; lakini yeche alisema, “Sistahili kuvifungua viatu vyake.”

¹⁵⁰ Lakini mara Yesu alipotokea, Yeye alikuwa na ishara, Nguzo ya Moto, Nuru juu Yake, kama hua alivyoshuka sauti ikisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, anayenipendeza sana.”

¹⁵¹ Angalia, ndipo Yohana mara akasema, “Hana budi kuzidi. Sina budi kupungua.” Yeye alilikabidhi Kanisa kwa Kristo. Amina.

¹⁵² Tunaambiwa ya kwamba, katika siku za mwisho, hilo litajirudia tena! Kutakuja Ujumbe, ambao utamtambulisha Masihi kwa watu. Na utakuwa katika namna hivi kwamba, watasimama wameduwaa kama walivyofanya wakati huo. Yeye aliahidi jambo hilo. Mlango unaofuata wa Mathayo, wa Malaki, unatwambia habari zake. Angalia.

¹⁵³ Waliuliza habari zake. Tabia ya Yohana ilimtambulisha katika roho ya Eliya. Sasa angalia manabii hao wawili.

¹⁵⁴ Sasa, Eliya alikuwa mtu aliyeinuka katika wakati wa Israeli, katika machafuko.

¹⁵⁵ Ahabu alikuwa ndiye mfalme. Na wanawake wote walikuwa wamedhihaki kama Yezebeli, na labda wamekata nywele mtindo wa kichwamaji na kadhalika, labda kama ilivyo kwetu siku hizi. Na wote walikuwa wamemfuata Yezebeli. Nao wachungaji wakawazia, “Hilo lilikuwa ni sawa tu. Waacheni. Acheni wafanye hivyo.”

¹⁵⁶ Na kwenye wakati huo, Mungu alimwinua mtu fulani kutoka nyikani, jina lake Eliya. Hata hatujui mahali alikotoka. Hakuwa na shule ya kumtambulisha. Bali aliinuka, naye akauhukumu upuuzi huo wote. Alihukumu mpangilio huo wote.

¹⁵⁷ Kama angejitokeza jukwaani, leo, angehukumu mpangilio wetu pia.

¹⁵⁸ Alimkemea kila Yezebeli. Na huyo, hatimaye, ndiye aliyemvunja moyo nabii huyo. Akakimbia, kama Yohana; akalala chini ya mretemu wakati Yezebeli alikuwa akitaka kumwua. Alimchukia.

¹⁵⁹ Ndipo tunakuta kwamba wakati Yohana alipokuja, kutoka nyikani tena, mpenda nyikani, akiwa na ujumbe wa moja kwa moja kwa wanawake wa kisasa wanaoishi wamepigwa talaka na kuolewa, na kuolewa tena, alikatakata kitu hicho vipande-vipande. Yeye hakutoka kwenye shule yoyote. Alitoka kwa

Mungu, mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Naye aliwakemea wanawake wa kisasa, aliwapinga vikali, wala hakuchezacheza nao. Bali alisema dhahiri, "Wakati ulikuwa umewadia, Masihi alikuwa anaenda kunena." Angalia jambo hilo.

¹⁶⁰ Sasa linganisha wakati wa kuja mara ya kwanza kwa Eliya na baadhi ya hawa manabii wa kisasa siku hizi, wakiwaachilia Mayezebeli wao wakate nywele zao, na kuvaal kaptura, kuvuta sigara, chochote wanachotaka kufanya, kuwaongoza huku na huko. Afadhali asiseme lolote, atamwacha, amchukue mwininge. Wanawaongoza huku na huko kwa kanuni za imani za kujibunia; hiyo ni aibu, mafundisho ya mwanadamu. Na, kwa kufanya jambo hilo, wanazibatilisha amri za Mungu, kwa kuwa wanaweza kuijunga na kanisa na huku wangali wakikiri kuwa ni Wakristo, na kushikilia haki zao na kusema wao ni Wakristo, na kuendelea. Hivyo ndivyo wanavyotaka. Hivyo ndivyo walivyofanya wakati huo.

¹⁶¹ Lakini, kumbukeni, ni kwenye wakati kama huo, kama vile Mungu alivyoahidi katika Malaki 4, ya kwamba angetimiza Neno tena. Hiyo ni kweli. Angalia mahali tulipo leo, kama tu ilivyokuwa katika siku za Yohana, kama tu ilivyokuwa katika nyakati hizo zingine.

¹⁶² Angalia maskini huyu Amosi akiinuka, maskini jamaa mzee. Hatujui mahali alikotoka. Alikuwa ni mchungaji. Mungu alikuwa akimpeleka kwenye malisho ya kondoo na malisho ya ng'ombe, na, na kumfundisha. Ndipo alipofika Samaria, na wakati alipoinuka na kusimama juu ya kile kilima siku hiyo, akaangalia chini kule. Na hilo jua likiangazia kichwa chake chenye upara, na masharubu yake yenyeye mvi, na amekaza macho yake na yanametameta. Macho yake matakatifu yalifumba na kufumbua, si kwa ajili ya mandhari ambayo watalii waliona walipofika mle, kwa sababu jiji lote lilikuwa limetumbukia dhambini.

¹⁶³ Ni nani mtu huyu maskini, asiyetambulika? Naam, ni Amosi, nabii. Alitabiri katika siku za Yeroboamu wa Pili, mfalme haini, aliyewaachilia watu kufanya lolote. Makuhani wote walikuwa katika jambo hilo. Walijenga makanisa mazuri sana. Walikuwa na nguo nadhifu mno. Wanawake wao walikuwa watovu wa uadilifu. Walivalia vyovoyote watakavyo. Watalii walisongamana kila mahali, kuwaona hao wasichana warembo na matendo yao.

¹⁶⁴ Ni Marekani nytingine tu ya kisasa, wanaodhaniwa ni watu wa Mungu. Hakuna mtu anayesema jambo lolote juu yake. Inaonekana kwamba ni mnaso mkubwa mno juu ya watu. Kumi na ta-...

¹⁶⁵ Miaka kumi na minane sasa, leo! Rebekah wangu ana umri wa miaka kumi na minane, leo. Miaka kumi na minane, nimevuka taifa hili, nikikemea vitu hivi. Na ninaporudi, mwaka

baada ya mwaka, kuna wanawake wengi zaidi waliokata nywele zao kuliko mara ya kwanza nilipoanza.

¹⁶⁶ Mhubiri mashuhuri, anayejulikana sana wa Kipentekoste alinipeleka chumbani, kama mwaka mmoja uliopita, mtu mzuri, anayejulikana sana, mtu anayejulikana kote ulimwenguni. Akasema mimi... “Ndugu Branham, hebu nikuwekee mikono na kukuombea.”

Nikasema, “Mimi si mgonjwa.”

¹⁶⁷ Akasema, “Lakini kuna kasoro fulani.” Akasema, “Ndugu Branham, utaiangamiza huduma yako. Hakuna mtu atakayeshirikiana. Si ajabu wahubiri hawatashirikiana nawe; ni jinsi unavyowakaripia hao wanawake.”

Akasema, “Hao watu wanakuuta nabii.”

Nikasema, “Kamwe sijasema mimi nilikuwa nabii.”

¹⁶⁸ Akasema, “Lakini wanafikiri ndivyo ulivyo.” Akasema, “Ninaamini jambo lile lile.” Akasema, “Wewe uliitwa ukawaombee wagonjwa.” Akasema, “Waombee wangonjwa, na uwaache hao wanawake peke yao. Unawaudhi.”

Nikasema, “Vipi?”

¹⁶⁹ Akasema, “Ukizungumza kuhusu wao kukata nywele zao na kadhalika.”

Nikasema, “Hilo ni kosa.”

¹⁷⁰ Biblia ilisema, “Mwanamke ambaye—ambaye hukata nywele zake, mumewe ana haki ta kumtaliki katika talaka.” Kweli kabisa. “Anaaibisha kichwa chake.” Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Sasa sijui kama unapenda jambo hilo ama hulipendi, bali hivyo ndivyo Biblia ilivyosema, katika Wakorintho wa Kwanza.

¹⁷¹ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh]...inabana mno mpaka ngozi iko nje. Na halafu wao—wao wanakuja huku, wanasesma, “Mbona, Bwana Branham, hizo ndizo aina tu za nguo wanazouza.”

¹⁷² Wangali wana bidhaa na cherehani. Hakuna udhuru. Wanawake wa Kiamishi na wa Kidunkardi wangali wanazivaa. Hakika. [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

Na ni jambo gani linalotukia? Wanatoka huko nje na kufanya yasiyofaa.

¹⁷³ Mwanamke mmoja alisema, “Vema, Bwana Branham, mimi sivai kaptura. Ninavaa s-...” Hizo ni nini, pedali su-... [Ndugu fulani anasema, “Visukuma pedali.”—Mh.] Naam. Kasema, “Ninazivaa.”

¹⁷⁴ Nikasema, “Hizo ni mbaya zaidi.” Nikasema, “Biblia inasema, ‘Ni chukizo kwa mwanamke kucaa vazi linalompasa mwanamume.’” Na Marekani hii ni tamasha inayoonekana chafu jinsi gani leo! Unaona? Hiyo ni kweli.

¹⁷⁵ Hebu nikwambie jambo fulani, dada. Huenda ukawa u safi kama yungiyungi, kwa mume wako ama kwa rafiki mpenzi wako mvulana, lakini kwenye Siku ya Hukumu utajibu kwa kufanya uzinzi. Yesu alisema, “Yeyote atazamaye mwanamke, kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye.” Kama mwenye dhambi huyo alikwangalia, naye mwanamke huyo atawajibika kwenye Siku ya Hukumu. Ulijianika mwenyewe kwake. Shauri yako. En-he.

¹⁷⁶ Mwanamke mcha Mungu angetaka kuвая jinsi hiyo kwa sababu gani? Kisha unadai kuва na Roho Mtakatifu ati kwa sababu ulinenе kwa lugha na kukimbia huku na huko sakafuni? Hilo, hata hivyo, nimewaona makafiri wakifanya hivyo, Wahotentoti. Roho Mtakatifu ni usafi, utakatifu, yasiyoghoshiwa. Hakika.

¹⁷⁷ Mtu huyu alisema, “Kama wewe ni... Wanakuamini wewe kwamba ni nabii. Kwa nini usiwafundishe jinsi ya kupokea karama kuu za kiroho, na jinsi ya kumfanyia Mungu mambo? Kwa nini usiwafundishe hayo kama wewe ni nabii?”

¹⁷⁸ Nikasema, “Ninawezaje kuwafundisha algebra wakati hata hawatajifunza ABC zao?” Mnajua ABC zinamaanisha nini? Daima Mwamini Kristo. En-he. Utafanyaje jambo hilo? Unaona, unataka kwenda *huko* juu sana, badala ya kuanzia *hapa* chini.

¹⁷⁹ Mungu atalijenga Kanisa Lake juu ya msingi wa Yesu Kristo, na hiyo ni Biblia. Nje ya hiyo, sehemu zingine zote ni mchanga udidimiao. Mungu habadiliki. Tabia Yake haibadiliki.

¹⁸⁰ Yeye aliwaumba wanawake tofauti na mwanamume, na mwanamume tofauti na wanawake. Aliwalisha tofauti, Naye anawataka wakae jinsi hiyo. Mnaona? Wanawake wanataka kuonekana kama mwanamume, na mwanamume anataka kuonekana kama wanawake. Loo, jamani! Ni upotovu wa jinsi gani! Ni...Na jambo hilo lote, linaonekana kana kwamba limewakaba watu, wala huwezi kulibadilisha. Linaonekana kama kwamba ni dubwana kubwa, weusi mkuu; kama mnaelewa na ninayonena habari zake, katika roho. Dude limewashikilia, nao—nao hawawezi tu kujitoa kwake; Hollywood chungu nzima, televisheni chungu nzima, upuuzi mwingine chungu nzima. Kila kitu tulicho nacho kimechafuliwa. Si ajabu, “Kazi isipokatizwa, kwa ajili ya Wateule, hakuna mtu atakayeokolewa.”

¹⁸¹ Ulicesma, “Sikujua jambo hilo hapo kabla.” Vema, sasa unalijua, tangu sasa na kuendelea. Unaona? Hiyo ni... Afadhali niache jambo hilo. Hebu turudi nyuma. Angalia.

¹⁸² Yohana alikuwa ni ishara. Na kumbuka ya kwamba, jinsi Mungu alivyolifanya mara ya kwanza, hivyo ndivyo atakavyolifanya tena. Aliahidi kufanya jambo hilo. Sasa, Mungu kamwe hajatumia kundi la watu, wakati wowote, kwa ajili ya jambo kama hilo.

¹⁸³ Kumbukeni, kulikuwako na kundi fulani wakati mmoja, ambalo, mtu mashuhuri aliyeitwa Ahabu, alijitwalia ninii... alijitwalia manabii mia nne wa Israeli. Sasa, hao hawakuwa manabii makafiri. Manabii mia nne wa Israeli. Wote walikuwa na digrii zao na kila kitu, walikuwa na shule kubwa.

¹⁸⁴ Kulikuwako na mtu mcha Mungu jina lake Yehoshafati, aliyekuwa mfalme wa Yuda, naye alishuka akaja kule. Na hapo ndipo mwaminio alipochangamana na asiyeamini. Mambo yakaenda kombo.

¹⁸⁵ Naye akasema, "Ramothi-Gileadi." Sasa angalia jambo hili, jinsi linavyoweza kuwa ni kweli. Yeye alisema, "Ramoth-Gileadi ni yetu, huko juu. Huko juu kwenye sehemu ile ya nchi kule juu, hiyo ni yetu." Yoshua, katika kuigawa nchi, aliwapa Israeli hiyo. Nao Wafilisti, makafiri, walikuja huko na kuwanyang'anya. Akasema, "Hiyo ni yetu."

¹⁸⁶ Sasa angalia jinsi ambavyo, kimsingi, watu wanaweza kuwa sahihi na hata hivyo kulikosa. Kitu hicho kweli kilikuwa ni cha Israeli. Lakini ahadi zote za Mungu, ndugu, zina masharti, unaona, "Kama wakitembea mbele za Bwana."

¹⁸⁷ Sasa angalia hapa. Yeye alisema, "Je, utaambatana nami, na kunisaidia kuirudisha nchi hiyo? Vema, hiyo ni, hao watoto wa Kifilisti wanayajaza matumbo yao kule, kwa ngano ambayo ni mali ya Israeli." Hilo ni kweli Kimaandiko. Yeye alisema, "Nisaidie kukwea kwenda huko na kuwapata."

¹⁸⁸ Kasema, "Vema, ninii yangu..." Hapo alifanya kosa baya sana. "Magari yangu ni yako, watu wangu ni sawa na wako. Nitaambatana nawe."

¹⁸⁹ Ndipo Yehoshafati akaanza kuwazia, mwajua. "Aisee, hivi haitupasi kumtaka shauri Bwana juu ya jambo hili kabla hatujaondoka?"

¹⁹⁰ "Loo, bila shaka," Ahabu akasema, "hakika. En-he. Samahani. I-ilinipasa kuwazia jambo hilo."

"Hivi hakuna nabii mahali fulani?"

¹⁹¹ "Loo, hakika. Nina—nina se—seminari yao hapa chini, wazuri sana uliopata kuona. Wote wanavaa mavazi yaliyo nadhifu sana. Hao ni wanazuoni walioelimika vilivyo. Nimewaelimisha, kikamilifu. Tutaenda kuwaleta."

¹⁹² Kwa hiyo wakashuka wakaenda kule. Nao wote wakakusanyika pamoja. Hawakuwa wanafiki. Waliomba na kuomba na kuomba, mpaka wakaona ono.

¹⁹³ Ndipo wakakaribia. Na mmoja wao akajifanya pembe mbili kubwa za chuma. Akasema, "Kwa hizi utawasukuma Wafilisti, ama Wa—Waashuri, moja kwa moja nje ya nchi." Akasema, "BWANA ASEMA HIVI. Kwea, Bwana yu pamoja nawe." Kila mmoja wao, wakati huo, kwa moyo mmoja, akaingia katika roho. Manabii wa Israeli wakasema, "Kwea, Bwana yu pamoja nawe."

Unasema, hayo ni Maandiko? “Mungu aliwapa watu urithi huu, naye adui anao. Una haki ya kwenda kuuchukua.”

Sasa, Mpentekoste, ninakutaka upate somo hapa.

¹⁹⁴ Lakini, Yehoshafati, akiwa ni mcha Mungu, akasema, “Kuna jambo fulani kasoro kidogo bado.” Kasema, “Je! huna mwengine mmoja zaidi?”

¹⁹⁵ “Ati mwengine mmoja, baada ya manabii mia nne waliofunzwa vizuri kusimama hapa?” Wengi kadiri ya walio kwenye orofa hii ya chini hapa. “Wamesimama katika moyo mmoja, wakisema, ‘BWANA ASEMA HIVI.’ Wakarejea nyuma, na kusema, ‘Yoshua alitupa nchi hii. Ni yetu. Nendeni mkaiteke!”

¹⁹⁶ Lakini Yehoshafati aliulizia mwengine. Kasema, “Je! hakuna mwengine tunayeweza kumtaka Bwana shauri kwa yeye?”

¹⁹⁷ Akasema, “Loo, yupo mwengine mmoja, lakini,” akasema, “Ninamchukia.” A-ha, a-ha. Kasema, “Yeye ni Mikaya, mwana wa Imla.” Kasema, “Ninamchukia. Yeye siku zote anasema mambo mabaya juu yangu.”

Kasema, “Mfalme asiseme hivyo. Nenda kamlete.”

¹⁹⁸ Ndipo wakawatuma wakimbajji fulani kule. Ndipo baadhi yao wakasema, “Sasa, Mikaya, ninataka kukwambia jambo fulani. Sasa, unajua walikufukuza, -kakuondoa kwenye ushirika, si muda mrefu uliopita, kwa sababu daima unasema mambo mabaya kwa watu. Sasa endapo unataka kurudishiwa kadi yako ya ushirika, wewe sema jambo lile lile wanalo sema, na, loo, wao watakuchukua moja kwa moja chini ya mkono wao.”

¹⁹⁹ Lakini ilitokea kwamba kweli yeye alikuwa ni nabii. Akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, nitasema tu yale Mungu anayoweka kinywani mwangu.” Loo! Mungu ambariki mtu huyo. Akasema, “Ngojeni mpaka usiku wa leo, nami nitaona yale Bwana atakayoniambia.”

²⁰⁰ Kesho yake asubuhi, akasema, “Kwea, bali nimeona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.” Ndipo akachukua ono lake na kulilinganisha na yale Eliya aliyo sema, kile kilichokuwa kimempata Ahabu. Angewezaje kubariki kile kilichokuwa kimelaaniwa? Haidhuru ni mara ngapi . . .

²⁰¹ Sisi ni taifa linalomcha Mungu. Kanisa la Kipentekoste, Kibaptisti, na Kimethodisti, na kadhalika, ni makanisa ya Kikristo, lakini unawezaje kubariki kile Mungu amelaani? Sijali, unasema, “Ni—nilijiunga na *hili*. Nilifanya *hivi*.” Hilo halina uhusiano wowote na jambo hilo. Angalia yale umefanya. Angalia Pentekoste, jinsi ambavyo wameachilia mambo. Angalieni jinsi mlivyo kuwa, na mwangalie jinsi mlivyo sasa. Si ajabu, macho ni, macho yamepofuka.

²⁰² Ndipo ye, Ahabu, ninii...Kasisi huyu alimpiga kofimdomoni. Ndipo akasema, "Mweke," naye Ahabu akasema, "mweke kule nyuma katika gereza la ndani. Nitakaporudi katika amani, jamaa huyu nitamshughulikia."

²⁰³ Akasema, "Kama kamwe ukirudi, Mungu hajasema nami." A-ha? Mnaona? Nabii alikuwa yupo hapo, ishara ilikuwa ipo hapo; hiyo hapo sauti Yake. Na, kushindwa kuitii, kulileta hukumu.

²⁰⁴ Roho Mtakatifu ndiye nabii wetu leo. Kutoisikiliza Sauti Yake? Yeye ametambulishwa katika Maandiko, ya kwamba angesema mambo haya. Yesu Kristo, katika umbo la Roho Mtakatifu!

²⁰⁵ Mungu alishughulika na mtu huyu mmoja. Huyu, Mungu kamwe hajishushughulishi na makundi; ni na mtu mmoja. Eliya hakuwa ni kundi. Yohana hakuwa ni kundi. Hawakuwa ni kundi wala dhehebu, si hata mmoja wao. Bali wote wawili walihukumu kitu hicho. Hiyo ni kweli. Yohana alisema, "Msiwazie kusema tuna Ibrahimu baba yetu. Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto."

²⁰⁶ Nay o ishara ya siku za mwisho itakuwa na Sauti ya wakati wa mwisho. Nay o ishara ya siku za mwisho itakuwa ni kulingana na yale yaliyotabiriwa katika Biblia. Nay o Sauti ya siku za mwisho, inayoifuata ishara ya siku za mwisho, itatambulishwa kabisa katika Maandiko, itakuwa ni Maandiko yaliyoahidiwa.

²⁰⁷ Sasa tumesoma katika Luka 17 ni kitu gani ishara ya wakati wa mwisho itakuwa, itakuwa kama ilivyokuwa kule Sodoma, ahadi. Na tuna Sodoma katika mambo ya kawaida, kwa nini hatuwezi kuamini ishara hiyo katika kiroho ipo hapa? Kama unaweza kuyaona Maandiko, pia, Luka 17 ndiyo hiyo ishara, na Malaki 4 ndiyo Sauti. Ishara ilikuwa ni kama Mungu akidhihirishwa katika mwili, akizijua siri za moyo; na Sauti ya Malaki 4 ilikuwa ni kuwaondoa watu kwenye kanuni zao za imani, kuwarudisha kwenye Imani ya baba zao. Hiyo ndiyo ishara.

²⁰⁸ Unajua nini? Ninafunga sasa. Ishara kwa kawaida zinakubaliwa, hakika; lakini, sauti, loo, la. Sauti inayoifuata ishara, hawataki uhusiano wowote nayo. Naam.

²⁰⁹ Ishara ya Yesu, kama Masihi, kuwaponya wagonjwa, waliikubali hiyo. Lakini siku moja Yeye alisema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja."

²¹⁰ Loo, jamani, sauti hiyo haikukubalika. Wao walisema, "Unajifanya Mwenyewe Mungu, sawa na Mungu."

Akasema, "Mimi ni Mwana wa Mungu."

²¹¹ "Loo, jamani, Mungu angewezaje kuwa na Mwana? Mnaona, hilo liwe mbali na Mungu kuwa na Mwana!"

²¹² Lakini, unaona, waliiamini ile—ile ishara, wagonjwa waliweza kuponywa, na, loo, hilo lilikuwa ni jambo zuri sana, hilo lilikuwa tu ni sawa kabisa. Lakini ilipofikia kwenye ile sauti, hawakutaka kuamini sauti hiyo. Walifanya nini? Walimfukuza.

²¹³ Na unajua nini? Biblia inatwambia, katika Ufunuo mlango wa 3, kwenye Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, ya kwamba Yeye angefanyiwa jambo lile lile. Alikuwa nje ya kanisa. Hilo ni Neno lililodhihirishwa. Alikuwa ni Neno lililodhihirishwa. Angali ni Neno lililodhihirishwa.

²¹⁴ Kama unaweza kuamini ishara ya Sodoma, ya Luka, kama unaweza kuiamini hiyo, basi kwa nini usiikubali Sauti ya Malaki 4? Unaona, kwa nini si wewe, wewe? Inaweza kuthibitishwa. Jinsi tu inavyoweza kufanywa ni... Ishara hiyo inaweza kuthibitishwa, bali inakubidi kuikubali ile Sauti.

²¹⁵ Musa aliagizwa ashuke aende kule, katika mambo ya kawaida, na kupata ishara ya kiroho na kuwaita watu wairudie ahadi ya baba zao.

²¹⁶ Malaki 4 ni kuwarudisha watu “Wairudie Imani ya baba zao.” Loo, rudini, Enyi vipofu mliotawanyika, makwenu!

²¹⁷ Katika kufunga, nitasema jambo hili, tamshi hili la mwisho. Nabii alisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Angalia, yeye alisema, “Kungekuwako na siku ambayo haingeitwa mchana wala usiku.” Sasa sikilizeni. Ninafunga. “Kutakuwako na siku...” Acha hili likolee ndani, na Mungu na aliweke katika kila moyo katika jamii hii, usiku wa leo, katika jumba hili la mikutano. Nabii alisema, “Kungekuwa na siku ambayo isingeitwa mchana wala usiku, kwa namna fulani ni siku ya utusitusi, ya mvua, yenye ukungu. Lakini,” kasema, “kwenye wakati wa jioni, kungekuwako Nuru.”

²¹⁸ Sasa, kumbukeni, jua daima huchomoza Mashariki na linaenda magharibi. Ustaarabu umelifuata jua. Mnajua jambo hilo. Na, angalieni, jua lile lile linalochomoza Mashariki ndilo jua lile lile linalotua Magharibi. Sasa, ustaarabu umesafiri pamoa na jua barabara, mpaka sasa Mashariki na Magharibi zimekutana. Tuko kwenye Pwani ya Magharibi; Mashariki na Magharibi.

²¹⁹ Na, kumbukeni, Injili imesafiri vile vile. Iliibuka huko Mashariki, kule kuja kwa Yesu Kristo, M-w-a-n-a, sio j-u-a. M-w-a-n-a, Mwana wa Mungu, aliibuka Mashariki, kwa watu wa Mashariki.

²²⁰ Na sasa kumekuwako na siku ambayo watu wamejiunga na kanisa, wakaunda madhehebu, mwanga tu wa kutosha kuona, “Vema, tutakuwa na kanisa. Tutajenga *hili*. Tutajenga shule. Tutajenga hospitali. Tutaelimisha. Tutakuwa na seminari.” Wamekuwa na nuru ya kutosha kufanya jambo hilo.

²²¹ Lakini, kumbukeni, Biblia ilisema, nabii wa Bwana, katika Biblia, ambayo ni BWANA ASEMA HIVI, “Jua lile lile lililoangaza Mashariki litaangaza tena Magharibi, wakati wa jioni. Itakuwa Nuru wakati wa jioni.”

²²² Yeye angefanya nini? Huyo anafanya vile vile hasa yale aliyosema katika Luka mlango wa 17. “Wakati wa mwisho, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa vile vile alivyofunuliwa Mashariki, Mwana yeye yule akiangaza, Nguvu zile zile, Roho Mtakatifu yeye yule, Jambo lile lile likifanya kitu kile kile. Itakuwa Nuru wakati wa jioni.”

²²³ Jua lile lile lililosafiri; M-w-a-n-a yeye yule amesafiri; akashuka kupitia Mashariki, kutoka kwa Paulo; akaruka akaingia Ujerumanii, juu ya Martin Luther; akaruka tena, kwenye mvuto wake mwingine; na akatoka huko akaenda Uingereza, kwa John Wesley; akaruka Bahari ya Atlantiki, hadi Marekani, kwa Pentekoste; na sasa Pentekoste imejififisha kabisa, nasi tuko katika Pwani.

²²⁴ Kila mmoja wao, aliunda madhehebu, kama tu walivyofanya pale mwanzo, waliunda madhehebu ambayo Mungu aliyalaani. Pentekoste, na hao wote, walifanya hivyo.

²²⁵ Bali Yeye alisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni. Kutakuwako na ishara itakayoinuka wakati wa jioni.” Msikose Hiyo, enyi marafiki. Msikose. Sasa, Mwana yeye yule angetoa Nuru ile ile. J-u-a lile lile linatoa nuru ile ile ya j-u-a. M-w-a-n-a yeye yule hutoa Nuru ile ile ya M-w-a-n-a.

²²⁶ Sasa, huo si msemo wangu. Kila mtu hapa, anayejua Biblia inasema jambo hilo, inueni mikono yenu. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo ni kweli kabisa.

²²⁷ Sasa, mnaweweza, ni juu yenu. Aminini ya kwamba Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, ameninii, yeye si mfu. Yeye yu hai. Yeye yuko katika unyenyekevu, mpole. Daima aliishi jinsi hiyo. Njia ya kupanda ni kushuka. Jinyenyekezeni, tokeni kwenye mawazo yenu magumu, na mkamwamini Bwana Yesu. Angalieni ile ishara, kisha mkaiamini ile Sauti. Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu!

Na tuinamishe vichwa vyetu.

²²⁸ “Na kama wasipoamini Sauti ya ishara ya kwanza, mkononi, kama ilivyokuwa na Musa, basi fanya ishara ya pili. Ndipo, kama hawataiamini ishara hii, basi chukua maji (maji yanawakilisha uhai) yaliyo katika bahari kuu ama baharini, ukayamwage ardhini, yatakuwa damu.”

²²⁹ Baba wa Mbinguni, tumechelewa sana sasa, bali Wewe uliahidi kutakuwako Nuru wakati wa jioni. Jalia Sauti ya Injili yetu izame ndani ya mioyo ya watu hawa, wanapoitafakari na kuisoma kwa Neno.

²³⁰ Ibariki jamii hii, Bwana. Wabariki watu hawa. Waangalie wameketi hapa, wana njaa, ni watoto wadogo maskini ambao wanapigwa na kusukumwa kila mahali, na *hili*, tukijua ya kwamba Shetani alifanya jambo hilo kusudi tu awapofushe wasilione jambo Hilo litakapofika pale. Wajalie, usiku wa leo, kwa moyo mmoja, wamwamini Yesu Kristo, waamini ahadi Yake, ya kwamba Yeye amefufuka katika wafu.

²³¹ Ulisema, “Wakati wasiotarajia, ndipo Mwana wa Adamu atakapokuja.”

²³² Mara wakati kanisa limepata ninii yake, lina thamani ya pesa nyingi zaidi, wakijenga mamilioni ya dola katika majengo. Wangekuwa heri, Baba, ninaamini, wamesimama huko nyuma pembeni, wakicheza ta—tari, wakiwa wameshika kofia mkononi mwao, ngoma ya kale pembeni kama Jeshi la Wokovu, kuliko jinsi ingekuwa kuketi katika nyumba hizi kubwa za maiti usiku wa leo, wakijaribu kujifananisha na ulimwengu, “Wakiwa na mfano wa utauwa, huku wakikana nguvu Zake.”

²³³ Tujalie, Bwana, usiku wa leo, mara nyingine tena, Bwana; kama vile Samsoni alivyosema kwa sauti kuu, “Mara nyingine tena, Bwana, mara nyingine tena.” Na ijulikane ya kwamba Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu; yeye yule jana, leo, na hata milele. Na ujitalbulishe mionganini mwetu, ili wapate kuona ile ishara, labda wataiamini ile Sauti. Katika jambo hili, ninaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²³⁴ Tutaitisha mstari wa maombi, upesi sana. Nimeona hakika sasa hivi ndio wakati tunapofumukana. Lakini hebu na tufanye mstari wa maombi, mstari mdogo tu wa maombi, ndipo tutaanza kesho.

²³⁵ Yeye alisambaza kadi za maombi leo. Kwa hiyo, tunasambaza kadi za maombi kila siku, kusudi kila mtu aweze kupata nafasi wanapokuja, wakati wa ajabu. Kuja huku kwenye mstari wa maombi, hilo halikuponyi. Mtu yeoyote anajua, katika kila mkuutano, wapo wengi wanaoponywa huko nje kuliko walio huku juu, unaona, daima. Roho Mtakatifu yuko tu kila mahali. Yeye anajaribu tu kuwapata waaminio, hivyo tu, anaoweza kuwafikia.

²³⁶ Sambaza kadi za maombi P, kama vile Paulo. Hebu, mahali tumekuwa... Vema, ita kutoka moja. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, acheni wasimame upande *huu*, mkiweza. Kadi yao ya maombi P, kama vile Paulo, moja mpaka kumi, simameni huku upande *huu*, kama unaweza kusimama. Endapo huwezi, basi tutapata mtu wa kukusaidia. Kumi; moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane... Vema, wawili zaidi. Nane, tisa, kumi, vema. Kumi mpaka kumi na tano, kumi mpaka kumi na tano, hao ni watano zaidi. Kumi na tano mpaka ishirini, simama kusudi niweze kuona kama unasimama; P, kumi na tano mpaka ishirini. Ishirini mpaka ishirini na tano. Hebu tuone sasa,

popote ulipo. Sasa hebu wengine katika kusanyiko wawe na kicho kweli kweli, dakika chache tu. Hiyo ingekuwa ni kadi ya maombi P, moja mpaka ishirini na tano. Sivyo? Ishirini na tano, moja mpaka ishirini na tano.

²³⁷ Sasa wengine wote wawe na kicho kabisa. Mpeni Mungu heshima kiasi hicho, upeni Ujumbe. Mnamwia Mungu hilo, kuangalia kwa muda kidogo na kutafakari.

²³⁸ Sasa nafikiri wanawaandaa watu. Hao ambaao hawaninii . . . Kama wana kadi ya maombi, wote hawajafanya mstari, watapata kujua; wataniambia katika dakika chache, halafu wataninii . . . ndipo tutaona kama labda mtu fulani ni bubu ama mtu ambaye hawezo.

²³⁹ Sijui ziko wapi, enyi marafiki, hizo kadi za maombi. Mvulana hushuka anakuja hapa . . . [Ndugu Branham anamwuliza mtu fulani jukwaani, “Ni nani aliyezisambaza? Ni wewe, ama Billy? Ati ni Billy?”—Mh.] Anaposhuka kuja huku, na kuzichanganya hizo kadi, mbele yenu enyi watu, kisha anakupa kadi ya maombi; anakuja moja kwa moja, anawaambia nyote mketi chini, anawapa kadi ya maombi. Mnaona? Sijui ziko wapi. Nimekuwa nikijaribu kumleta mtoto huyu huku juu, mnaona. Na, zingine, si—sijui habari zake, si—sina njia ya kujua hilo. Nadhani Mungu hulitaka tu jinsi anavyotaka kuliarnisha namna hiyo.

²⁴⁰ Sasa, sasa wengine wenu, ambaao hamna kadi ya maombi. Inua mkono wako, useme, “Sina kadi ya maombi, bali mimi ni mgonjwa.” Inua mkono wako, popote humu jengoni. Sijali uko wapi, inua ninii wako . . . Vema, hakuna watu wengi sana hapa basi, sasa. Vema, kulingana na hilo, haitakuchukua muda mrefu sana kuombea mstari wa maombi sasa kesho. Wapo kama ishirini humu ndani, bila wale wanaosimama hapa, ambaao ni wagonjwa.

²⁴¹ Hilo ni zuri. Nina furaha kukuona ukilikubali jinsi hiyo. Ulikuwa na imani zaidi kuliko nilivyodhani ulikuwa nayo, labda. Unaona? Unaona? Kama ulikubali uponyaji wako, ukaitupilia mbali kadi yako, Mungu akubariki. Hiyo ni imani halisi ya kweli. Hakuna mtu aliyejukwekea mikono; ulimwekeea Kristo mikono.

²⁴² Sasa ninyi hapa usiku wa leo, ambaao hamtakuwa kwenye mstari wa maombi, aminini hadithi hii. Kama yule mwanamke aliyegusa upindo wa vazi Lake, Naye akageuka na kutambua ya kwamba alimgusa, ni wangapi wanaokumbuka hadithi hiyo? Hakika, mnaikumbuka.

²⁴³ Sasa mnaamini jambo hilo, Yeye, Biblia ilisema katika Waembrania 4, ya kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuchukuana na mambo ya udhaifu wetu”? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hivi Yeye si angetenda vile vile? [“Amina.”] Hivi Yeye si amefanya jambo hili, usiku baada ya usiku, hapa? [“Amina.”] Ni wangapi wamekuwa katika

mikutano mingine na kumwona Yeye akifanya jambo hilo? Inueni tu. [“Amina.”] Hakika. Mnaona? Kote ulimwenguni! Yeye anajua, anajua yote kukuhusu.

²⁴⁴ Sasa mnaona jambo ninalojaribu kufanya. Ni wangapi wanaofahamu yale ninayojaribu kufanya? Mnaona? Ninawatakeni, bila mtu yejete kuwawekea mikono, ninawatakeni, kama bidhaa halisi ya Mungu, mseme, “Yesu Kristo, ninakuamini. Sasa ninakukubali kama mponyaji wangu. Sasa ninakukubali kama Mwokozi wangu. Ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote, ni kazi iliyokwisha.” Basi shikilieni ahadi hiyo, shikilieni maungamo yenu na msonge mbele nayo. Angalieni litakalotukia. Mnaona? Angalieni litakalotukia. Mnaona? Sasa hilo ndilo ninalojaribu kuwafanya mfanye, jinsi hasa tunavyopaswa kuamini.

²⁴⁵ Ungesema nini? [Mtu fulani anasema, “Nne na kumi na tisa.”—Mh.] Namba nne, kadi ya maombi namba nne na namba kumi na tisa, hazipo. Kadi ya maombi namba nne. Mwangalie mtu fulani; angalia kadi ya jirani yako. Kadi ya maombi namba nne na namba kumi na tisa. Vema, hebu kidogo, ngojeni. Mnaona, kama nisipomwita, basi ninapata mwangwi kwa jambo hilo, mnaona. Wasemaje? Wasemaje? [“Nne.”] Umepata nne? Vipi kuhusu tisa... Kumi na tisa haipo bado. Wasemaje? [“Pamoja na nne.”] Kadi ya maombi namba nne haipo bado, ama kumi na tisa. Kama mtu anazo hizo kadi, naomba mje mstarini. Ama, angalia, unaona, huenda ikawa... hivi ninii... Hivi maskini mtoto huyo mchanga ana kadi? Angalieni, si ninii... Hiyo siyo ile namba. Je! mama *huyu* hapa ana kadi, kwenye kiti hiki cha magurudumu? Angalia hiyo namba. Je! hiyo—hiyo ndiyo namba yake? Bibi aliye kwenye machela, en-he? Wameipata. Wao, zote ziko sasa. Sawa. Vema. Sasa—sasa, ninyi watu mlion na kadi ya maombi, zishikeni. Tutahudumu, kwa neema ya Mungu.

²⁴⁶ Sasa, enyi marafiki, kwa kuwa huu ndio usiku wa mwisho tutakaokuwa nao, kesho ni Jumapili alasiri, hebu na tujitilize. Sasa chukua kila kutokuamini uliko nako na kila—kila wazo lolote lisilo la busara, na kuliweka chini sakafuni, na kulikanyanga kwa mguu wako, kama tusemavyo. Useme, “Bwana Yesu, nitakuamini Wewe.” Ni wangapi watakaofanya jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Asante. Mungu awabariki.

²⁴⁷ Sasa mtu yejete asiondoke. Ketini kimya kabisa, na mwamini. Angalieni huku, na sasa angalieni.

²⁴⁸ Utambulisho wa Mungu daima umekuwa ni kujua, unaweza kuona kile kimekuwako, na kusema kile kimekuwako, na jinsi hilo liliyvo, ama kile kitakachotukia. Tunajua jambo hilo. Hivyo ndivyo manabii walivyojulikana. Hivyo ndivyo Yesu alivyojulikana kama Masihi. Naye ni Masihi yeye yule leo kama alivyokuwa wakati huo, ila tu bila mwili wa kawaida hapa duniani. Yeye alimtuma Roho Wake aje autumie mwili

wako, mwili wangu. Sasa, huenda usiweze kufanya jambo hili. Tunajua, katika Maandiko, kuna mmoja katika kizazi kimoja. Lakini, unaona, bali hata hivyo unaweza kuamini jambo hilo, nawe una mambo mengine unayoweza kufanya, kila mtu.

²⁴⁹ Vipi kama kidole changu kikiamua, ati kwa sababu hilo si jicho langu, hakitakuwa kidole changu tena? Vipi kama mkono huu ukisema, “Sitainuka tena, maana kama mimi si jicho, wala sikio, sitakuwa mkono”? Mbona, ingeulemaza mwili wangu.

Wewe kuwa kile Mungu alichokuweka uwe.

²⁵⁰ Ni mara ngapi nimemstaajabia Oral Roberts, Billy Graham, Tommy Osborn!

²⁵¹ Baadhi ya hao watu wanaingia mle na kusema, “Utukufu kwa Mungu! Aminini!” Imani ya kulazimisha. Wanaondoka, wanatoka hapo wakiwa wazima sana wawezavyo kuwa.

²⁵² Billy Graham anasimama na ujumbe, na kuzungumza na watu dakika chache, anasema, “Toa uamuji wako; njoni madhabahuni.” Anasimama tu pale, hasogei tena.

Alisema, “Kwa hiyo kwa nini unafanya hivyo, Billy?”

²⁵³ Kasema, “Ujumbe wangu ulienezwa. Unatoka kwa Mungu.” Hiyo ni kweli.

²⁵⁴ Yeye yuko kwenye hilo kanisa la Sodoma, jinsi tu inavyopaswa kuwa hasa. Jina lake likiishia kwenye h-a-m kutoka Ibrahim, herufi sita; Abraham zilikuwa saba. Mnamwona mjumbe wa kanisa hilo, huko chini Babeli? Hakika. Hakuna mtu nchini anayeushikilia ujumbe huo wa toba, kama Billy Graham. Anasimama pale. Anaondoka hapo, anaenda kula nyama choma kisha anaenda kulala, anakunywa maziwa ya mgando. Hiyo ni sawa.

²⁵⁵ Na wakati inapokubidi kusimama na kupigana na pepo! Wakati mmoja huko Long Beach, mimi pamoja na Ndugu Jack... Baba yako alikuwa amesimama pale.

²⁵⁶ Na hapo alisimama Bw. Fuller, Charles Fuller, ndugu mzuri, amesimama pale akihubiri. Yapata watu elfu mbili ama elfu tatu pale alasiri hiyo. Tuliketi kwenye mkutano wake tukasikiliza. Nilikuwa nimekodi chumba cha mikutano, nyuma yake. Naye alisimama pale na kutoa mahubiri mazuri. Kisha akasema, “Yupo mtu ye yote hapa aliyetaka kumkubali Kristo?” Watu wawili ama watatu wakashuka wakaja kwa ajili ya kuwekwa wakfu kwa watoto wao wachanga. Mwanamke mmoja akasema alitaka kumkubali. Akaja na kufanya ombi dogo, mmoja wa hao mashemasi, akarudi akaketi chini. Wakapeana mikono, wakageuka na kutoka nje. Hilo hapo kundi lake la watu wenye elimu, waliovaa nadhifu, likitoka nje pale.

²⁵⁷ Hawa hapa wangu wanaingia, wenda wazimu, viti vy a magurudumu, vipofu, viwete, vilema, walemavu. Wakati imani yako inapokabiliana na kitu kama hicho!

²⁵⁸ Sasa hapa, nimedai kwamba Kristo ni nani? Na sasa wasioamini wameketi hapo, wakitaka kupata kosa moja, mnaona, wakijaribu kupata tu kosa moja.

²⁵⁹ Kumbukeni, hapa si muda mrefu uliopita kule Toronto, tulikuwa tumesimama pale tukihubiri, tukiwaombea wagonjwa. Niliendelea kuhisi roho ngeni; alikuwa ameketi kwenye mkono wangu wa kushoto. Niliendelea kumwangalia. Kulikuwako na mtu aliyekuwa ameketi hapo, kundi fulani lilikuwa limemkodi aje mle ndani kunipumbaza akili. Angezunguka kwenye kambi za majeshi na kuwafanya askari watembee kwa mikono yao na kubweka kama mbwa, na kadhalika; upumbazaji wa akili. Nilimhisi pepo huyo mchafu. Sikujua alikokuwa akitokea. Nikaendelea kuangalia. Nikaona hicho kivuli cheusi. Nilingojea tu dakika chache. Nikasema, “Ewe mtoto wa Shetani, ni kwa nini ibilisi amepofusha moyo wako kwa kitu kama hicho? Kwa kuwa umekuja kumteka Mungu, kumsai Roho wa Mungu, watakubeba wakutoe hapa.” Alipooga papo hapo kitini mwake na angali amepooza. Mnaona?

²⁶⁰ Hatuigizi kanisa. Ni wangapi wamekuwa mikutanoni na kuona mambo kama hayo yakindeka, mnajua mambo ambayo hutinende? Hakika. Hiyo ni kweli. Kumbukeni, i—iweni na kicho.

Sasa huyu hapa, nafikiri, mtu wa kwanza. Hiyo ni kweli?

²⁶¹ Sasa, mnaona, nimehubiri, nikawaambia lile hasa lililopaswa kutukia katika siku hii. Sasa hilo ni ishara, kama likitukia. Hivyo ndivyo ile ishara ilivyokuwa, basi aminini ile Sauti inayoifuata ishara hiyo. Unaona?

²⁶² Sasa huyu hapa mwanamke. Hasa, kwenu ninyi wageni, hii ni Yohana Mtakatifu 4, ambapo Bwana wetu Yesu alikutana na mwanamke kisimani. Hawakuwa wamekutana hapo kabla, maishani, Naye akamwambia mwanamke huyo shida yake ilikuwa ni nini. Naye akatambua ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi. Mnajua hadithi hiyo? Hii hapa tena, mwanamume na mwanamke wanakutana. Sasa yeze siye mwanamke huyo, wala mimi siye Mwanamume huyo, bali huyo angali ni Mungu yeze yule. Unaona? Sasa, Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya,” Yohana Mtakatifu 14:12.

²⁶³ Sasa, mama, bila kukujuua, sina fununu ni kwa nini umesimama pale. Huenda ikawa ni shida ya nyumbani. Huenda ikawa ni kwa ajili ya mtu mwininge. Labda wewe ni mgonjwa. Labda ni...Labda umesimama hapo, ukijifanya tu. Kama ndivyo, ona tu kitakachotukia. Unaona? Labda unaiga kitu fulani. Chochote kile, sininii mimi... Huenda ukawa mwaminio halisi. Hilo sijui mimi, bali Mungu anajua. Lakini utajua kama Yeze alikwambia kweli au la, sivyo? Kama ni kweli, utajua jambo hilo.

²⁶⁴ Sasa, unaona, hivyo ndivyo imani yako inavyopaswa. Ungetakaje kuja hapa? Sasa kama mtu ye yeyote anaamini ya kwamba si kweli, njoo hapa na kumchukua mgonjwa huyu, njoo hapa na kuwachukua hawa wengine. Basi kama hutafanya hivyo, basi usinilaumu. Unaona?

²⁶⁵ Sasa angalia hapa, dada, kwa dakika moja tu. Sasa sina fununu, sijui chochote kukuhusu wewe. Wewe ni mwanamke tu anayesimama hapo.

²⁶⁶ Sasa kama Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Ambaye nimemthibitisha kwa Biblia, aliahidi ya kwamba Yeye angerundi katika siku za mwisho na kujifunua Mwenyewe katika utimilifu wa Roho Wake.

²⁶⁷ Ni kama tu Kanisa linavyokua; kama vile linavyokuja kutoka mwanadamu, kote kote kutoka miguuni, linakuja kwenye mapaja, linafika kichwani, na kichwa ndicho kinachouongoza mwili. Nao ule Mwili umekua, tangu Kanisa la kwanza, ukapanda moja kwa moja, katika haya, katika matengenezo, limepanda juu mpaka sasa. Limepitia kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sasa ni Kichwa (Kristo) kikija kwenye ule Mwili, Mwili wa Kristo. Yeye Ndiye anayejua. Mkono wangu haujui kutenda kazi, ni kwa kichwa changu tu. Lakini Yeye Ndiye anayejua, hiyo ndiyo sababu Yeye ni Neno.

²⁶⁸ Mimi si Neno. Mimi ni mwanadamu. Lakini, mnaona, Yeye anautumia mwili huu. Kwa sababu, Yeye alikuwa apate kuutakasa mwili huu, kusudi apate kuutumia, na kutoa karama. Ni kama tu kuvuta gia, ndipo Roho Mtakatifu anashika hatamu.

²⁶⁹ Ndipo, kama atakuelezea ama kukwambia yale umefanya, kile kilichokuleta hapa, ama jambo fulani kukuhusu wewe, utaamini jambo hilo. Na je! kusanyiko litaamini vile vile? [Kusanyiko linasema, "Amina." —Mh.] Bwana Mungu na alijalie.

²⁷⁰ Sasa nachukua kila roho, humu ndani, chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sasa kaeni kimya. Msisogee-sogee.

²⁷¹ Angalia hapa, dakika moja. "Niangalieni mimi," kama walivyosema Petro na Yohana, walipopitia kwenye lile lango. Kwa maneno mengine, sikilizeni tu yale ninayosema. Unaona?

Yesu alimwuliza mwanamke huyo maswali machache. "Nipe maji ninywe."

²⁷² Unaona, nimekuwa nikihubiri, jambo lile lile. Baba alinituma ha—hana Baton Rouge. Niko hapa.

²⁷³ Baba alisema alikuwa na haja kupitia Samaria. Aliketi pale. Mwanamke ndiye aliye kuwa wa kwanza kumjia. Alifanya ishara hiyo moja kwa mwanamke huyo, na mji wote ukatubu. Ni tofauti jinsi gani . . .

²⁷⁴ Unawazia, kama angefanya jambo lile lile, usiku wa leo, unafikiri Baton Rouge yote ingetubu? Ninatilia hilo shaka,

nawe je? Hakika ninalitilia shaka. Lakini tuko katika siku za mwisho, wakati uovu umekuwa mwovu mno kuliko ulivyopata kujulikana.

²⁷⁵ Sasa hali zako. Uko hapa upate kuombewa. Kweli kabisa. Nawe una ugonjwa wa koo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Si hilo tu, bali yupo mtu unayemwombea. Ni mtoto, na mtoto huyo ana ugonjwa wa koo. Na ni shida ya koo la mtoto huyo, ni vivimbe kooni. Je! unaamini ya kwamba Mungu atamponya, pia? Leso hiyo iliyo mkononi mwako, ambayo umemwinulia Mungu, kama ushahidi. Usilitilie shaka sasa. Nenda ukaweke hiyo leso juu ya mtoto huyo. Usilitilie shaka, kwa moyo wako wote. Mungu atawaponya nyote wawili na kuwafanya wazima. [Dada huyo anasema, "Asifiwe! Haleluya!"—Mh.] Unaweza kufanya hivyo? ["Yesu! Asante, Yesu!"] Basi nenda, na Bwana awe pamoja nawe. ["Utukufu kwa Mungu! Haleluya!"]

U hali gani? Hatufahamiani, pia.

²⁷⁶ Je! Unaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ndiyo ishara. Sasa Sauti, ni, "Rudini kwenye Neno!"

²⁷⁷ Sikujui; Yeye anakujua. Kama ataniambia jambo fulani kukuhusu wewe, basi utaamini ya kwamba Neno hilo ambalo nimesema litathibitishwa? Huo—huo ndio uthibitisho Walo. Unaona? Nilisema yeye alifanya jambo hilo; huko ni kutabiri. Sasa kama unabii huo ukitimia, basi Yeye alisema, "Usikieni."

²⁷⁸ Una ugonjwa mbaya sana wa wasiwasi ambao unaugua, wasiwasi. Pia una kivimbe, na kivimbe hicho kiko mguumi mwako. Hiyo ni kweli, sivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Sasa je! unaamini? ["Ndiyo, bwana."] Basi nenda zako, na uamini. Na, jinsi umeamini, ndivyo itakavyokuwa kwako.

²⁷⁹ U hali gani? Sikujui, bali Mungu anakujua. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida zako? Ningalie. Una shida. Lakini kwa kweli unasimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine, na huyo ni yule aliyelelewa pamoja nawe. Ni dada. Hiyo ni kweli. Sasa unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia huyo dada yako ana shida gani? Utakubali jambo hilo? Ana ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Je! unaamini ataponywa sasa? Basi, kulingana na imani yako, na iwe kwako.

²⁸⁰ Njoo, mama. U hali gani? Kama Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini, ama yale uliyofanya, ama jambo fulani, je! litakufanya uamini? Unajua ya kwamba mimi ni... si—si—sikujui. Hiyo ingekuwa ni tabia Yake ikijitambulisha Yenyewe ndani yangu, kulingana na Neno ambalo Yeye aliahidi. [Huyo dada anasema, "Nitaliamini tu."—Mh.] Unaamini jambo hilo? ["Ndiyo. Amina."]

²⁸¹ Wewe ni mwingine, una shida ambazo mwanamke wa umri wako angekuwa nazo, bali wazo lako kuu ni juu ya mtu mwingine. Shauku yako kwa Mungu; unamtafuta Mungu si kwa

ajili yako mwenyewe, bali kwa ajili ya mtu mwingine, ambaye ni mwanamume. Ni mume wako. Naye ana ugonjwa wa moyo. Je! unaamini ya kwamba Yeye ataninii... Mungu atamponya? Nenda, liamini. Na, jinsi ulivyoamini, ndivyo itakavyokuwa kwako.

²⁸² Sasa, unaona, mahubiri yote, kwa saa hiyo niliyokuwa nikihubiri. Hicho, chochote kilichokuwa, watu watatu ama wanen wamepit, sasa ni vigumu kwangu kusimama hapa. Unaona? Unaona, umati wote unaonekana tu kama rangi ya maziwa maziwa, humu ndani. Unaona? Yesu alisema, "Nguvu zilinitoka." Na kama mwanamke mmoja, kwa kugusa vazi Lake, alimtoa nguvu, Naye ni Mwana wa Mungu; na mimi je! mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yake?

²⁸³ Yeye alisema, "Mambo niyafanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya. *Zaidi ya haya mtayafanya.*" Ninajua Mfalme James inasema, "kubwa kuliko." Lakini kama utachukua tafsiri asili, ilisema, "*Zaidi ya hizi mtazifanya.*" Hakuna mtu angaliweza kufanya kubwa zaidi. Yeye aliwafufua wafu, na akakomesha maumbile, na kufanya kila kitu. Lakini Yeye alisema, "*Zaidi ya hizi mtazifanya,* maana ninaenda kwa Baba."

²⁸⁴ "Ulimwengu hautaniona; bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi..." Angalia, "Mimi," mimi—mimi ni kiwakilishi nafsi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu." Basi, si mtu huyo. Ni Kristo.

²⁸⁵ Ninasema jambo hilo, kwa namna fulani kujitikisa kidogo, kwa namna fulani kujaribu kujirudia. Unafikia kiwango ambapo baada ya kitambo kidogo... Si wakati ukiwa pale *juu*, wala hapa *chini*; ni katikati. Ni wangapi wanaofahamu jambo hilo? Ninajua mna—mnafikiri mnafahamu. Na mimi, pia.

²⁸⁶ Je! ulipata kujua ya kwamba washairi na manabii daima wana hamaniko la moyo? Ni wangapi wanajua jambo hilo?

²⁸⁷ Ni wangapi waliowahi kusoma juu ya William Cowper, yule mshairi mkuu Mwingereza? Mnajua, aliandika, "Kuna chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye vena za Imanueli." Baada ya kuandika wimbo huo, je! mlisikia kilichompata? Nilisimama karibu na kaburi lake si siku nyingi zilizopita. Alijaribu kujiua, na akajitosa mtoni.

²⁸⁸ Ni wangapi waliopata kusikia juu ya Stephen Foster, aliyeipa Marekani nyimbo zake zilizo bora sana za jadi? Alikuwa nazo kichwani wala si moyoni. Kila wakati uvuvio ulipomgusa, angeandika wimbo. Ndipo wakati uvuvio ulipomwacha, hakujua la kufanya na nafsi yake, naye alichanganyikiwa kabisa. A—a—alikuwa akinywa pombe mfululizo. Na hatimaye wakati alipoanza kutoka katika uvuvio huo, alimwita mtumishi wake, naye akachukua wembe akajiua. Hiyo ni kweli.

²⁸⁹ Mwangalie Eliya, yule nabii. Alipanda akaenda kule na kuita moto kutoka mbinguni; akaita mvua kutoka mbinguni

kwenye siku ya kwanza; na akazifunga mbingu na kufanya hayo yote. Ndipo wakati uvuvio ulipomwacha, alienda huko nyikani na akatamani kufa. Ndipo Mungu akampata, siku arobaini baadaye, ameingia ndani ya pango. Hiyo ni kweli?

²⁹⁰ Mwangalie Yona, yule nabii. Baada ya kutoa ujumbe wake, alikwea akaketi chini kilimani, na akamwomba Mungu amruhusu afe. A-ha. “Ruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani.”

²⁹¹ Watu hawafahamu jambo hilo. La, la, hamtaelewa. Wala mimi siwezi kulielezea, wala hakuna mtu mwингine anayeweza. Huwezi kumwelezea Mungu. Mungu hajulikani kwa utafiti wa kisayansi. Mungu anajulikana kwa imani. Tunamwamini. Unawezaje kuelezea? Ingekuwaje ni imani, tena? Tunamfahamu Mungu kwa imani.

²⁹² Kanisa kamwe halitajua ile kazi na uchovu, na kazi ngumu na majaribu, mambo ambayo yamejaribu kuuleta, Ujumbe. Yeye anafahamu. Thawabu yangu haitoki kwa watu.

²⁹³ Angalia hapa, mama. Naam, upesi. Mwanamke huyo ana uvuli wa mauti. Mungu asipomjia mwanamke huyu mara moja, ninaweza kuona... Hivi hamwoni ule weusi unaoning'inia kumzunguka? Atakufa, hapana shaka kamwe. Hapa si muda mrefu uliopita, walipiga picha ya kitu kama hicho, na ninayo nyumbani. Yeye ana uvuli mweusi unaoning'inia karibu naye. Ametiwa uvuli wa mauti.

²⁹⁴ Maskini mama huyu amefanyiwa upasuaji. Na katika upasuaji huu, walimfanya upasuaji wa kansa. Na sasa yeye ana shida, kila namna ya—ya, vema, magonjwa ya ziada. Jambo moja, wewe ni mnyonge sana huwezi kusimama. Jambo lingine, usaha unatokea kwenye kibofu. Sasa, ili kwamba ujue tu ya kwamba sisemi tu jambo fulani. Unaona? Hiyo ni kweli. Lakini, mama, daktari alijaribu. Ninampa heshima kwa jambo hilo. Lakini, yeye alikuwa ni tiba, lakini Mungu ndiye mponyaji. Utakufa namna hiyo. Yeye amekwisha kufanya yote aliyoweza kufanya. Je! unaamini? [Huyo dada anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Njoo hapa, kwa dakika moja.

²⁹⁵ Kwa agizo nililopewa na Mwenyezi Mungu, likashuhudiwa kwangu na Malaika, ambaye yupo sasa katika umbo la Nguzo ya Moto, ninamkemea ibilisi huyu anayeyachukua maisha ya mwanamke huyu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nenda, amini sasa. Kwa yote yaliyo ndani yako, amini.

²⁹⁶ Una shida inayowaua watu wengi zaidi kuliko kitu kingine chochote, ugonjwa wa moyo. Wanadai ya kwamba ndio ugonjwa namba moja, bali sio, bwana. Dhambi ndiyo ugonjwa namba moja wa kuamini. Je! unaamini ya kwamba Yeye anaweza kuuponya huo moyo na kukupa afya? [Huyo ndugu anasema, “Ninajua Yeye anaweza.”—Mh.] Basi nenda, amini hilo. Mungu akubariki.

²⁹⁷ Unafikiri Mungu anaweza kuuponya mgongo wako na kukufanya mzima? Je! unaamini kwa moyo wako wote? Nenda, amini hilo, dada. Angalia kinachokupata, utapata nafuu.

²⁹⁸ Yabisi kavu na ugonjwa wa moyo. Lakini unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukupa afya? [Dada anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Kwa moyo wako wote? [“Ndiyo, bwana.”] Utalikubali? [“Ndiyo, bwana.”] Kulingana na jinsi ulivyoamini, hivyo ndivyo itakavyokuwa kwako. Sasa nenda, amini kwa moyo wako wote, na Mungu atakuponya.

²⁹⁹ Wewe pia una ugonjwa wa mgongo. Je! unaamini ya kwamba Yesu Kristo anaweza kukuponya? [Dada anasema, “Ndiyo, bwana.”] Nenda sasa, amini kwa moyo wako wote. Siwezi kukuponya, unaona.

³⁰⁰ Tezi kibofu, wasiwasi, na pia una yabisi kavu. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukupa afya, kukuponya? Unakubali jambo hilo? Nenda, na uamini, basi.

³⁰¹ Linakufanya uwe macho mara nyingi sana, kukoho. Bali Mungu huponya pumu. Unaamini hilo? [Ndugu huyo anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Je! unaamini Yeye anakuponya sasa? [“Naam, bwana.”—Mh.] Mungu akubariki. Asante, kwa ajili ya imani yako.

³⁰² Vipi kama hata sikutamka neno kwako, nilikuwekea tu mikono yangu, je! ungeamini? [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Njoo hapa. Ninakuwekea mikono yangu, katika Jina la Yesu Kristo, na hebu yabisi kavu ikuache. Inakuacha.

³⁰³ Njoo. Njoo, dada. Je! unaamini? [Dada anasema, “Ndiyo, bwana. Nilikwisha ponywa na Bwana hapo kabla.”—Mh.] Vema, hilo ni jambo zuri sana. [“Haleluya!”] Basi nenda ukale chakula chako cha jioni basi, na tumbo lako litakuwa sawa. [“Haleluya! Haleluya! Haleluya!”]

³⁰⁴ Shida nyingi sana za mgongo, umekuwa ukikusumbua kwa muda mrefu. Nenda, ukiamini wewe ni... Nenda, ukiamini utapona, na Mungu atakufanya jambo hilo. [Ndugu anasema, “Mungu ameniponya. Amina.”—Mh.] Amina. Hivyo ndivyo inavyotakiwa. [“Bwana asifiwe.”] Bwana akubariki, ndugu. Amina.

³⁰⁵ Kisukari si kitu, kwa Mungu kuponya. Anaweza kuwaponya. Unaamini jambo hilo? [Dada huyo anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Vema. Likubali, na nenda ukamwamini sasa kwa moyo wako wote.

³⁰⁶ Wewe pia unao katika damu yako. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Nenda, amini kwa moyo wako wote, na upone.

³⁰⁷ Unaamini Yeye alikuponya wakati hiyo ilipokugusa? Alikuponya.

³⁰⁸ Ugonjwa wa wanawake. Ugonjwa wa moyo. Unaamini hilo? [Dada anasema, “Naliyamini.”—Mh.] Nenda, u—ukaponywe katika Jina la Yesu.

³⁰⁹ Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya mgongo wako, mafigo yako yatakuwa . . . Akubariki! Nenda tu moja kwa moja.

Mimi siponyi. Siwezi kuponya. Mimi si mponyaji.

³¹⁰ Ulifikiri nini wakati Yeye aliposema kuhusu mgongo wake, je! unaamini wako uliponywa, pia? Vema, nenda tu, ukiamini hilo, ndipo . . . Nenda tu ukaliyamini, kwa moyo wako wote.

³¹¹ Wako pia, je! unaamini ya kwamba Mungu anakuponya? Nenda, amini, kwa moyo wako wote. Mungu atakujalia kama wewe . . . Inakupasa kuamini, hata hivyo.

³¹² Je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, pia? [Dada huyo anasema, “Bwana asifiwe! Hakika ninaamini.”—Mh.] Vema, Mungu akubariki. Songa mbele tu na uamini kwa moyo wako wote.

³¹³ Njoo, bwana. Maskini tone jeupe likitona chini. Utambuzi wa hilo ungeonyesha kisukari. [Ndugu huyo anasema, “Kisukari.”—Mh.] Je! unaamini ya kwamba Yeye atakuponya? Hebu twende Kalvari sasa kwa ajili ya kuwekewa damu. Kwa imani, katika Jina la Yesu Kristo, na aponywe. Amina. Mungu akubariki, ndugu. Amini kwa moyo wako wote. Je! unaamini? [“Kweli kabisa.”]

³¹⁴ Vipi kuhusu baadhi yenu katika wasikilizaji sasa? Je! mnaamini kwa miyo yenu yote, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

³¹⁵ Vipi kuhusu wilaya *hii*? Maskini mama anayeketi, akiniangalia moja kwa moja pale, akiugua ugonjwa wa wanawake, je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Umehaa koti dogo tu la bluu. Vema. Amini sasa, Yesu Kristo anakuponya. Ni rahisi tu jinsi hiyo.

³¹⁶ Mama anayeketi moja kwa moja nyuma yako, nywele nyeusi. Yeye alisema, “Asante, Bwana.” Kitu fulani kilimgusa. Hakujua kilikuwa ni Kitu gani. Ugonjwa wa kibofu ulikuacha, ukiketi papo hapo, papo hapo nyuma ya mama aliyeponywa wakati uo huo. Kama unaamini kwa moyo wako wote hapo, mama. Unaamini? Vema, inua mkono wako kama unataka kuukubali. Mungu anakuponya.

Vipi kuhusu hili hapa chini, mtu fulani *hapa* ndani?

³¹⁷ Huko nyuma kwa wasikilizaji, sasa kwa uchaji sana. Msisogee. Mnaona, magonjwa haya yatatoka kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine.

³¹⁸ Vipi kukuhusu wewe, bwana? Huyu mzee anayeketi hapa kwenye kitu hiki? Unaamini? Unaamini Mungu anaweza kukuponya? Yabisi kavu, na una mkamba. Unaamini ya kwamba

Mungu atakuponya huo? Unaamini? Vema, unaweza kupata ulichoomba. “Kama unaweza kuamini!”

³¹⁹ Unafikirije, mama, unayeketi karibu naye? Unaamini, pia? Unaamini? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Uko mbali sana nami. Mwamini tu sasa. Unaamini nimekwambia Kweli? Basi presha yako ya damu iliyopanda itashuka. Unaamini jambo hilo?

³²⁰ Uliinua mkono wako, pia. Ulikuwa ukijaribu kumtia moyo. Unaamini Mungu anaweza kuniambia nini... Umekuwa mwema sana kumsaidia, sasa Mungu atakuwa mwema kukusaidia. Una shida ya kiroho ambayo imekuwa ikikusumbua. Kama hiyo ni kweli, tikisa mkono wako namna *hii*. Itatatuliwa sasa. Yeye analinyosha.

³²¹ Ni wangapi wanaoamini? Ni wangapi wenu watakuba-... amba si Wakristo, wana—wana hisia ya kwamba Yesu Kristo yupo hapa, amba wangetaka kusimama sasa, waseme, “Yesu, ninetaka kujitambulisha kama mwenye dhambi, je! utanisamehe dhambi zangu?” Simama kwa miguu yako. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni... Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Hili, Yeye anakuona. Anaandika jina lako unapofanya hivyo.

³²² Upande huu kwenye roshani, simameni, mseme, “Bwana Yesu, ninataka kuninii, ninataka kutambulishwa. Ninataka rehema kwa ajili ya nafsi yangu.” Mungu akubariki, bwana. “Ninataka rehema, Bwana Yesu.”

³²³ Hivi huwezi kuona, ewe rafiki, ya kwamba ni Yeye hapa? Mungu akubariki, ewe kijana. Mungu akubariki. Mungu akubariki, msichana. Hilo ndilo jambo kuu kabisa ulilopata kufanya. Sasa mtu mwingine ambaye hajafanya jambo hilo, simama, useme, “Ninataka kutambulishwa, Bwana Yesu. Ninajitambulisha mwenyewe, usiku wa leo.”

³²⁴ “Yeye atakayekiri dhambi zake, atapata rehema. Yeye anayeficha dhambi zake, hatafanikiwa.”

³²⁵ Utafanya hivyo, Mbele Zake? Mungu akubariki, mama. Ninataka... Mungu akubariki. Naam. Na Bwana akubariki. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Bwana akubariki.

³²⁶ Unasema, “Je! hilo linamaanisha lolote?” Kati ya mauti na uzima, hiyo ndio tofauti.

³²⁷ Je! mnatambua Uwepo Wake hapa? Mnautambua huo? Mnauhisu huo? Mnaona, mnauona, mnauona ukitenda kazi. Huyu ni Yeye. Hivyo ndivyo vile hasa alivyosema angefanya. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.—Mh.]

³²⁸ Mtu mwingine aseme, “Ninataka kujitambulisha kama mwenye dhambi, Bwana. Nisamehe dhambi zangu sasa.”

Kama tayari umesimama, inua tu mkono wako. Wengine wenu mnaosimama kwenye kuta, inueni... Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mtu mwininge aseme, huko juu kwenye roshani upande wa nyuma, aseme, "Ninataka kujitambulisha, Bwana Yesu. Ninaomba rehema, usiku wa leo, katika Uwepo Wako wa Kiungu, nikiamini ya kwamba, Mungu ye ye yule atakayenihukumu, Uwepo Wake upo hapa sasa. Yeye anajua ya kwamba anasema na moyo wangu na kuniambia ya kwamba nimekosea. Ninataka kusimama na kusema ya kwamba nimekosea. Ninakiri makosa yangu. Unanihukumu, moyoni mwangu." Hiyo ndiyo sababu nilisimamisha mstari wa maombi. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

³²⁹ Unafikiri niliusimamisha huo kwa sababu gani? Niliusimamisha kwa sababu nilijua hilo lilipaswa kutukia.

³³⁰ Sasa, kuna wengine hapa, hivi hamtasimama? Simama na useme Kitu fulani kinasema na moyo wako, umekosa. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. "Nimekosa. Nisamehe, Bwana. Ninajitambulisha mwenyewe. Ninasimama. Bwana, katika Uwepo Wako. Ninajua Wewe upo hapa. Mimi... Huna budi kuwa hapa. Ulisema hili litakuwa ndilo ja-jambo ungefanya. Sasa mimi nakuwa... . Ninaona ile ishara, nami ninajua nimeelezewa kwamba hiyo inapaswa kuwa ndiyo ishara ya siku hii. Ninaisikia Sauti iliyotuita kwenye toba. Mimi hapa, Bwana. Ninaamini ishara hiyo. Ninaisikia hiyo Sauti."

³³¹ Hiyo Sauti inasema nanyi sasa! Geukeni, Ninyi mliotawanyika! Geuka, Ewe nyota inayozurura! Geukeni, Enyi mlio fukuzwa! Geukeni, usiku wa leo!

³³² Hivi huwezi kugeuka? Simama tu na useme, "Ninajitambulisha mwenyewe kama mwenye dhambi, nikiomba rehema." Hivi utafanya hivyo, mtu mwininge? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, huko juu, mwanangu. Nikikukosa, Yeye hatakukosa. Mungu akubariki, mama. Hilo ni safi sana. Hilo ni sawa kabisa. Mtu mwininge? Endelea tu... . Ninataka kushikilia kwa dakika moja zaidi, kwa sababu ningali ninasikia mzigo mdogo hapa, mnaona. Mtu mwininge? Mungu akubariki, mama. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Ndiyo hiyo. Mtu mwininge, "Ninataka kujitambulisha mwenyewe, nisimame mwenyewe tu na kusema nimekosea. Ninaomba rehema"? Utafanya jambo hilo? Upesi sana kabla hatujaenda mbali zaidi, simama na useme, "Ninataka kujitambulisha mwenyewe, Bwana Yesu." Mungu akubariki, msichana.

³³³ Unajua, labda kabla hujafika nyumbani, lakini wakati fulani ama mwininge kutakuwako na ukungu baridi ukija usoni mwako. Labda asubuhi fulani daktari atakuja na atasikiliza mapigo yako ya moyo yakipitia kwenye mkono wako wa shati, hakuna kitu kingine kingeweza kufanywa. Ndipo utahisi

mawimbi baridi ya mauti yakielea usoni mwako. Utakumbuka yale umefanya.

³³⁴ Kumbuka, hawawezi kukuzika chini sana, hawawezi kukufanya chochote. Mungu aliahidi, "Nitakufufua tena, katika siku ya mwisho." Angalia. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Mtu na asugue Hilo likutoke kama ukiweza. Yesu Kristo alisema jambo Hilo. "Yeye aaminiye, hiyo ni kusema, afahamuye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, hataingia Hukumuni, kuhukumiwa, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Kwa sababu, amemwamini Mwana wa pekee wa Mungu, ambaye Mungu amemfufua, miaka elfu mbili iliyopita, na yu hai hapa, usiku wa leo, akionyesha sifa Zake za kufufuka Kwake.

³³⁵ Kungekuwako na mwingine atakayesimama, baada ya hilo, mwingine aseme, "Ninataka kulikubali. Ninataka kumkubali." Mungu abariki. Mungu akubariki. Hilo ni zuri sana, msichana. Hilo ni jambo la kishujaa. Ninawatakeni mwone.

³³⁶ Niliangalia wito wa madhabahuni, hapa wakati fulani uliopita, watu wakija, wakitafuna chingamu, wakipigana-pigana mangumi ubavuni.

³³⁷ Lakini mliona uaminifu kwenye nyuso za watu hao? Hao wasichana, hata baada ya kuwakemea juu ya nywele zao zilizokatwa, kujipodoa; wakiwa wamejipodoa, na nywele zilizokatwa, walismama papo hapo vivyo hivyo, "Mimi ni mwenye dhambi. Nirehemu, Mungu." Hiyo hapo ile mbegu imekaa pale. Nuru iliimulikia, nao wanajua. Mungu awabariki.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

³³⁸ Ninamtaka kila mwaminio hapa, ambaye amesimama karibu na mtu huyo aliyesimama, uweke mkono wako juu ya mtu huyo, (utauweka?), huyo aliyesimama. Walikuwa wamesimama karibu na wewe. Kama wewe ni Mkristo, weka mkono wako juu, juu ya dada, ndugu, "Nimeweka mkono wangu juu yako sasa. Nitaomba."

³³⁹ Baba wa Mbinguni, kuna wale hapa usiku wa leo amba—ambao wanakuamini. "Mbegu zingine zilianguka karibu na njia," Wewe unasema, "ndege wakaja na kuziokota. Zingine zilianguka penye mawe, na miiba na michongoma. Lakini zingine zinaenda penye udongo mzuri, wenye rotuba." Na Uwepo Wako ukiwa hapa, usiku wa leo, umewashawishi wengi hapa usiku wa leo ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, ya kwamba Wewe U hai milele. Nawe umeahidi, kwa kuwa U hai, sisi nasi tunaweza kuishi pia.

³⁴⁰ Bwana Yesu, waliamka na kusimama kama ushahidi ya kwamba walikuamini. Sasa, Bwana, ninajua ya kwamba Wewe utawatetea katika Siku ile. Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi

Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia waende kwenye kanisa zuri na wabatizwe katika ubatizo wa Kikristo. Jalia wajijunge na kundi zuri la waaminio. Jalia wajazwe na Roho Mtakatifu. Jalia wawe kumbukumbu za Injili, vito katika taji Lako kwenye Siku ile. Na kama nisipowaona tena ng'ambo hii ya ile Siku kuu, jalia niwaone Siku ile kama katika lile ono, wakisema, "Hivi hunikumbuki? Ilikuwa kule Baton Rouge, usiku ule, ambapo nilisimama." Tujalie, Baba. Hao ni Wako, kupitia Jina la Kristo.

³⁴¹ Hapa kuna ninii, iliyowekwa mbele zangu, katoni ya leso, vijiatu, buti, leso, na nguo, na aproni. Tunafundishwa, katika Biblia, ya kwamba walitoa kutoka katika mwili wa Mtakatifu Paulo, leso na aproni, pepo wachafu wakawatoka watu. Sasa, Baba, tunajua ya kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali ni Mungu yeye yule, kwa hiyo ninaomba ya kwamba Wewe utatujalia matokeo yale yale, kwa kuwa kizazi hiki kinaamini kwa uaminifu. Wao hawakumwamini Paulo ati kwa sababu yeye alikuwa ni Paulo; walimwamini Paulo kwa sababu Wewe ulijitambulisha Mwenyewe na Paulo. Sasa wao wanaamini jambo lile lile usiku wa leo, Bwana, ya kwamba umetambulishwa mionganini mwetu, usiku wa leo. Na siku moja, tunasema ninii . . .

³⁴² Mwandishi mmoja alikuwa akitwambia, ya kwamba, "Israeli walikuwa wakienda zao kwenye nchi ya ahadi, nayo Bahari ya Shamu ikawakabili, kuwatenganisha na nchi ya ahadi." Mwandishi huyo alisema, ya kwamba, "Mungu aliangalia kupitia kwenye ile Nguzo ya Moto, kwa macho yenye hasira, wakati ilipoenda juu ya Israeli. Ilifanya upofu, giza kwa wasioamini, na nuru kwa Israeli. Na wakati hiyo Bahari ya Shamu ilipowakabili, ilihofu, ndipo ikafingirika na kurudi nyuma, nao Israeli wakavuka kwenda kwenye nchi ya ahadi juu ya nchi kavu."

³⁴³ Bwana Mungu, angalia chini usiku wa leo, kupitia Damu ya Yesu Kristo, Mwanao. Ninapoweza mikono yangu juu ya leso hizi; wakati zitakapowekwa juu ya wagonjwa, jalia Roho Mtakatifu, Bwana, amwangalie mtu huyo, na jalia ugonjwa uondoke humo, na jalia wavuke waingie katika nchi hiyo ya afya njema na nguvu. Hivyo, Biblia ilisema, "Juu ya mambo yote," ya kwamba walitaka kwamba "tuwe na afya yetu." Lijalie, Bwana. Ninawatuma, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

. . . nitafuata
 Aniongozapo . . . (hebu tuimbe tu) . . .
 nitafuata,
 Nitaambatana Naye, (sasa Uwepo Wake upo
 hapa, hebu tu tumwabudu katika wimbo,
 kwa utamu), kote.

³⁴⁴ Je! Mnaweza kuuimba kweli namna hii?

Aniongozapo nitafuata,
 Aniongozapo nitafuata,
 Aniongozapo nitafuata,
 Nitaambatana (ukitaka, sasa inua mkono
 wako), pamoja Naye kote.

Na tusimame sasa, inueni mikono yenu tena.
 . . . Naye bustanini,

³⁴⁵ Kila mtu na aimbe kwa Roho sasa. Ujumbe wa kukatakata kweli. Na tumwabudu katika Uwepo Wake. Yeye hupenda kuabudiwa.

. . . bustanini,
 Nitaambatana Naye bustanini,
 Nitaambatana Naye, Naye kote.

³⁴⁶ Sasa hebu na tuuvumishe. “Ninaweza . . .” Sasa wakati unapofanya hivyo, ninataka upeane mikono na mtu fulani, useme, “Mungu akubariki, ewe msafiri. Mungu akubariki, msafiri,” namna hiyo. Sisi tu kitu kimoja mmoja na mwenzake. Mmethodisti, na Mbatisti, Mpresbiteri, Wapentekoste, wote wapeane mikono wao kwa wao. “Mungu akubariki, msafiri.” Hivyo ndivyo tulivyo: wasafiri.

. . . bustanini,

³⁴⁷ Mungu akubariki, msafiri. Mungu akubariki. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaendelea kupeana mikono. Sehemu tupu kwenye kanda.—Mh.]

. . . bustanini,

Sasa hebu na tuinue mikono yenu.

Nitaambatana Naye, Naye kote.

³⁴⁸ Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa unyenyekevu, katika maombi. Msisahau, asubuhi, shule ya Jumapili.

³⁴⁹ Kwa namna moja ama nyingine, ninahisi tu Uwepo wa Mungu ukiwa halisi sana moyoni mwangu. Ni vigumu sana kwangu kuondoka, usiku wa leo, kwa namna fulani. Ninajisikia Roho Mtakatifu amefurahi, usiku wa leo. Huenda tukawa na mkutano mzuri sana kesho, tukiwaona watu wakimjia Kristo, mnaona. Mtu fulani alishangaa ni kwa nini sikutoa wito wa madhabahuni. Ninangojea mpaka niongozwe kuufanya. Mnaona?

³⁵⁰ Ninatumaini ya kwamba kila mtu aliyeinua mkono wao, ama aliyesimama, ninatumaini ya kwamba utakuwa kwenye kanisa zuri kesho, kuchukua mahali pako mionganoni mwa waaminio.

³⁵¹ Wakati vichwa vyetu vimeinamishwa, nitamwomba mchungaji hapa aje mbele, akiweza, akaturuhusu tufumukane. Mungu awabariki sasa, huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa mbele za Mungu.



SAUTI YA ILE ISHARA SWA64-0321E
(The Voice Of The Sign)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ultolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 21 Machi, 1964, katika Shule ya Sekondari ya juu ya Denham Springs huko Denham Springs, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org